
Ijumaa Novemba 20, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580405
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**BIBI** wa miaka 95 afariki dunia kwa kushambuliwa na mbwa

UKURASA 3



**UKOMO** matumizi vifungashio plastiki sasa Desemba 31

UKURASA 3



**Mancini kupanga kikosi cha Italia ni kazi**

UKURASA 21

# KIKOSI KAZI

• **Vijana**, sura mpya zatawala Baraza la Mawaziri Zanzibar, Serikali Umoja wa Kitaifa kitendawili... *Endelea ukurasa. 2*



## SURA MPYA

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji,** Mudrik Ramadhan Soraga

**Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi,** Abdallah Hussein Kombo

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi,** Rahma Kassim Ali

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango,** Jamal Kassim Ali

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,** Masoud Ali Muhammed

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo,** Soud Nahoda Hassan

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale,** Lela Mohamed Mussa

**Waziri wa Maji na Nishati,** Suleiman Masoud Makame

**Waziri wa Habari, Vijana na Utamaduni,** Tabia Mwita Maulid

## WAKONGWE

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Wakaazi**, Riziki Pembe Juma

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali**, Simai Mohamed Said

**Waziri wa Nchi , Ofisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora**, Haroun Ali Suleiman

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi**, Dk. Khalid Mohammed Salum

## Mbaroni tuhuma matukio kigaidi

UKURASA 3



## Uwekezaji Simba utata mtupu

UKURASA 2



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

MICHEZO KAZE ATANGAZA DK. 180 ZA HATARI UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Sura mpya vijana zang'ara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, ameunda Baraza la Mawaziri lenye sura nyingi mpya, wakiwamo vijana wengi.

Katika baraza hilo, ameunda wizara 15 tofauti na baraza lililopita lililokuwa na wizara 14, huku akiwateua mawaziri 13 kuziongoza wizara hizo na mbili kuziweka kiporo. Wizara hizo ni za Biashara ya Viwanda, na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto. Sambamba na uteuzi wa mawaziri wa wizara hizo, kati ya mawaziri 13 aliowateua, wanawake ni wanne na wizara zote hizo zitaongozwa na mawaziri bila kuwa na naibu mawaziri.

Akitangaza uteuzi huo, jana, Ikulu mjini Zanzibar mbele ya waandishi wa habari, Dk. Mwinyi alisema ameteua mawaziri pekee kuongoza wizara kwa sababu kwa sasa hakuna haja ya kuwa na manaibu waziri.

Mawaziri wakongwe walioteuliwa ni Haroun Ali Suleiman, ambaye anakuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora. Haroun ni Waziri pekee aliyedumu nafasi ya uwaziri kwa miaka 20 tangu mwaka 2000 akianzia Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Amali.

### SURA MPYA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji ni Mudrik Ramadhan Soraga ambay Mwakilishi wa Bububu na kabla ya kugombea uwakilishi alikuwa Balozi Mdogo wa Tanzania nchini Comoro.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Masoud Ali Muhammed, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ni Jamal Kassim Ali na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo anakuwa Soud Nahoda Hassan.

Waziri wa Habari, Vijana na Utamaduni ni Tabia Mwita Maulid na Wizara ya Maji na Nishati ni Suleiman Masoud Makame. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale ni Lela Mohamed Mussa wakati Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi anakuwa Rahma Kassim Ali.

Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi ni Abdallah Hussein Kombo.

### SURA ZA ZAMANI

Mbali na sura mpya, pia kuna sura zilizozoeleka katika baraza la mawaziri akiwamo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk Khalid Mohammed Salum.

Pia yumo Riziki Juma Pembe ambaye sasa anakuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Katika serikali iliyopita alikuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

### UMOJA WA KITAIFA

Wakati Rais Dk. Mwinyi alitangaza baraza la Mawaziri, amesema hadi juzi alikuwa hajapokea taarifa kutoka ACT Wazalendo kama kitaingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hivyo kuunda baraza kupitia chama kimoja cha CCM licha ya Katiba kuruhusu kuwamo katika muundo huo.

Alisema alishakiandikia barua chama hicho kuwasilisha majina ya wateule wa uwakilishi wa viti maalum pamoja na jina la Makamu wa Kwanza wa Rais lakini bado hakijarejesha majibu.

"Tokea nilipotangazwa kuwa Rais wa Zanzibar nilisema niko tayari kuendeleza maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na wezetu tumeshaandikia barua lakini bado hawajajibu chochote. Kwa vile bado muda upo pengine watajibu," alisema Dk. Mwinyi.

Kwa mujibu wa Katiba na Zanzibar, chama kitakachopata zaidi ya asilimia 10 kitashirikiana na chama kilichoshinda kuunda serikali, katika uchaguzi huo, mgombea Urais wa Zanzibar kupitia ACT Wazalendo, Maalim Seifa Sharif Hamad, alipata asilimia 19.1.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa ACT-Wazalendo, Salim Bimani, alikiri kupokea barua ya kutakiwa kuwasilisha jina la Makamu wa Kwanza wa Rais na kwamba suala hilo litaamuliwa katika vikao vya juu vya chama hicho.

"Bado chama kinaendelea na vikao vyake vya ndani ili kujibu barua iliyowasilishwa kuhusu kuteua jina la Makamu wa Kwanza, hivyo chama kikishaamua tutawaiteni waandishi wa habari ili kutoa tamko la kuingia au kutoingia katika serikali," alisema. Bimani.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar bado muda upo ambao ni siku 90 tangu Rais kuapishwa.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Jaji mstaafu Joseph Warioba (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja mradi wa Apopo Tanzania, Dk. Georgies Mgode (kushoto), kuhusu namna panya wanavyofundishwa kutegua mabomu chuoni hapo jana. Wa (pili kulia) ni Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

## Mfanyabiashara adai jina 'Rais wa Tanga' ni ukarimu

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MFANYABIASHARA Yanga Omary Yanga, maarufu kama Rais wa Tanga, amedai mahakamani kwamba anaitwa rais kwa sababu ya ukarimu wake na kwamba haina uhusiano na tuhuma zinazomkabili za kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine gramu 1052.63.

Jana Mahakama Kuu, Kanda ya Tanga, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu Mahakama ya Mafisadi, iliyoketi chini ya Jaji Imakulata Banzi, ilisikiliza mahojiano kati ya mshtakiwa na Jamhuri baada ya kujitetea.

Wakili wa Serikali Constantine Kakula, alimuhoji mfanyabiashara huyo kwamba jina la rais wa Tanga linahusiana na kazi yake ya kusambaza dawa za kulevya.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano hayo kati ya Wakili Kakula na Yanga;

**Wakili Kakula:** Mshtakiwa wewe unajulikana hapa Tanga kama Rais wa Tanga, ni kweli?

**Yanga:** Ni kweli, watu wananiita hivyo.

**Wakili Kakula:** Kwa hiyo umeridhika kuitwa hilo jina?

**Yanga:** Mimi nawasikiliza na wananiongelea hivyo hata watangazaji kwenye vyombo vya habari.

**Wakili Kakula:** Kwa hiyo mpaka kwenye vyombo vya habari (redio) umesikia wanakuita hivyo?

**Yanga:** Kweli nimesikia wananiita hivyo.

**Wakili Kakula:** Ni sahihi nikisema kuwa wanakuita rais wa Tanga kwa kuwa ni msambazaji wa dawa za kulevya?

**Yanga:** Sijawahi kufanya biashara hiyo na wala sitafanya.

**Wakili Kakula:** Umewafanyia nini kikubwa wananchi mpaka wakuite rais?

**Yanga:** Hakuna kubwa nililowafanyia ni kwa sababu ya ukarimu wangu tu kwa watu.

Awali akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Majura Magafu, mfanyabiashara huyo aliiambia mahakama kuwa anafanya biashara halali iliyompatia mapato ya kutosha ya kuuza kwa bei ya jumla bidhaa mbalimbali, ambayo humpatia karibu Sh. milioni moja kama faida kwa siku.

# Uwekezaji Klabu ya Simba ni utata mtupu

**Na Mwandishi Weu**

TUME ya Ushindani (FCC), imeibua utata uliosababisha ucheleweshaji wa mchakato wa kubadili mfumo wa uendeshaji wa Klabu ya Simba, huku ikikanusha madai yao kwamba tume ndiyo chanzo cha sakata hilo.

Pia utata huo, kwa mujibu wa FCC, unatokana na uteuzi wa mtendaji mkuu wa Simba kuteuliwa kabla ya uwekezaji kufanyika pamoja na kiasi kilichokubaliwa katika uwekezaji huo kutolewa.

Katika taarifa yake kwa umma jana, FCC ilisema ucheleweshaji huo unatokana na mwitikio hafifu wa kampuni ya Simba Sports Club Company Limited kuwasilisha taarifa kamili na kwa wakati mbele ya Tume katika kufanikisha uchunguzi.

Taarifa hiyo ilikanusha madai yaliyotolewa na Msemaji wa Klabu hiyo, Haji Manara, na Mwekezaji wa Klabu hiyo, Mohamed Dewji, maarufu Mo Dewji, kwamba mchakato huo wa mabadiliko umekwamia FCC.

Kwa mujibu wa FCC, Aprili 24, mwaka jana, ilipokea ombi kutoka Simba la kupatiwa mwongozo wa kisheria chini ya Sheria ya Ushindani kuhusu namna ya kushughulikia mchakato wa mabadiliko unaohusisha kampuni za Simba Sports Club Holding Company Limited, Mo Simba Company Limited na Simba Sports Club Company Limited.

Ilisema FCC ilifanya vikao viwili baina ya Simba Sports Club Company Limited hadi Julai 24, mwaka huu ambapo wadaawa walionekana kuelewa mwongozo wa kisheria na kuahidi kuutekeleza kama walivyokubaliana na tume.

Baada ya ukimya wa muda mrefu wa wadaawa, Tume ilisema iliutoa mwongozo wake kama ilivyoombwa na wadaawa walitarajiwa kwa mujibu wa sheria, na kuleta maombi husika kwa tume yaliyomo kwenye mwongozo wa FCC.

Hata hivyo, ilisema katika ufuatiliaji wake wa kila siku, walibaini viashiria kuwa klabu ya Simba inaongozwa na Simba Sports Club Company Limited chini ya uenyekiti wa Mohamed Dewji kabla ya wadaawa hawajawasilisha maombi yao ya muungano mbele ya tume.

"Kitendo hiki, kwa mujibu wa mwenendo wa uchunguzi wa masuala ya ushindani ni kiashiria cha uvunjifu wa kifungu cha 11 (2) cha Sheria ya Ushindani, hivyo, Januari 23, 2020, tume ilianzisha uchunguzi kuhusu jambo hili kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani," ilieleza.

Taarifa hiyo ilisema wakati uchunguzi ukiendelea, Julai 23, mwaka huu, tume ilipokea maombi ya muungano wa kampuni kutoka kwa wadaawa, wakijulishwa nia yao ya kuichukua klabu ya Simba na kuiendesha kama kampuni chini ya kampuni mpya waliyoianzisha ya Simba Sports Club Company Limited.

"Tume iliyafanyia uchambuzi wa awali maombi hayo na Julai 20, mwaka huu, tume iliwajulisha wadaawa kwamba taarifa walizowasilisha mbele yake (FCC) hazikukidhi matakwa ya Sheria ya Ushindani, hivyo kuwataka wawasilishe taarifa husika ili mchakato wa uchambuzi uendelee," ilisema taarifa hiyo.

Kadhalika taarifa hiyo ilisema kuwa Oktoba 13, mwaka huu, tume ilisitisha kwa muda mchakato wa uchambuzi wa maombi ya muungano wa kampuni na kuwajulisha wadaawa.

"Madhumuni ya kusitisha huko ni kupata taarifa na ufafanuzi zaidi toka kwa wadaawa na wadau wengine. Kwa mfano, taarifa zilizoombwa na tume kutoka kwa uongozi wa Klabu ya Simba ni pamoja na ufafanuzi kuhusu uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba kabla ya uwekezaji kufanyika; kiasi halisi ambacho mwekezaji," ilifanua.

## HABARI KITAIFA

# Vifungashio plastiki mwisho Desemba 31

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa hadi Desemba 31, mwaka huu kuwa ni siku ya mwisho ya utumiaji wa vifungashio vya chupa za maji, karanga au ubuyu, biashara inayofanywa na wachuuzi wadogo.

Akizungumza na waandishi wa habari za jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hivi karibuni limekuwako ongezeko la uzalishaji wa vifungashio vya plastiki ambavyo chanzo chake hakijulikani na ni vifungashio ambavyo havina kibali cha Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Alisema utengenezaji, usambazani na matumizi ya vitu hivyo ni uvunjaji wa Kanuni Na 3 na 4 za Sheria ya Mazingira ya 2004, kanuni ambazo zilitungwa na kutangazwa 2019 ili kutekeleza katazo la serikali la matumizi ya plastiki.

Kanuni namba 3 inawataka wazalishaji kuwa na kibali kutoka TBS baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa, lakini hali haiko hivyo kwa sasa," alisema Dk Gwamaka, na kuongeza kwamba kuwapo kwa vifungashio hivyo sokoni ni kinyume cha kanuni ya 4 (b) na (c) ambayo imetungwa na kutangazwa ili kulinda afya ya binadamu, wanyama pamoja na mazingira dhidi ya athari zinazoweza kujitokeza.

Kwa mujibu wa kanuni za upigaji marufuku mifuko ya plastiki, ni marufuku kutengeneza, kuuza, kusafirisha ndani na nje ya nchi, kusambaza na kutumia mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa za aina yoyote.

Kwa mujibu wa kanuni hizo, baraza lazima lisimamie sheria na kuzuia matumizi ya bidhaa zisizoruhusiwa kisheria, alisema Dk. Gwamaka.

**Utengenezaji, usambazani na matumizi ya vitu hivyo ni uvunjaji wa Kanuni Na 3 na 4 za Sheria ya Mazingira ya 2004, kanuni ambazo zilitungwa na kutangazwa 2019 ili kutekeleza katazo la serikali la matumizi ya plastiki.**

# Mbaroni madai kuhusika matukio ya kigaidi

**Na Edwin Mhagama**

JESHI la Polisi nchini, linawashikilia watu kadhaa kwa madai ya kuhusika katika matukio ya kigaidi mkoani Mtwara na Cabo Delgado nchini Msumbiji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP), Simon Sirro, alisema wamepata ushahidi kuwa baadhi ya vijana ambao wamekimbilia Msumbiji kujiunga na kikundi hicho cha kigaidi ni Watanzania na kuwataka raia wema kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

Sirro alisema taarifa itatolewa endapo wataona baadhi ya watu wanaonesha mienendo isiyofaa yenye lengo la kujiunga na kundi hilo.

"Kuna watu tumewakamata wanakiri kwamba wamehusika na yale matukio ya Mtwara. Nitoe rai kwa wazazi wa maeneo yale kwamba kuna vijana wanatumika maeneo ambayo yako mpakani, hivyo niwaombe sana Watanzania tukemee sana hili. Mtoto wako akijiingiza maisha yake yatakuwa hatarini kwa sababu ni kundi baya na majibu yake huwa ni mabaya pia,"alisema.

IGP Sirro alisema vijana kutoka mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo Kigoma na Mwanza, wamekuwa wakienda Msumbiji kujiunga na kikundi hicho cha kiuhalifu na kuwataka wakazi wa Mtwara na Watanzania kwa ujumla kutokuwa na wasiwasi na usalama wao kwa kuwa jeshi hilo limeimarisha ulinzi.

"Wananchi waendelee kusaidia familia zao wasiwe na woga. Kuna watu tumewakamata kutoka Kigoma na Mwanza wanasema wanakwenda Msumbiji kuungana na lile kundi, kundi lile lengo lao ni baya," aliongeza IGP Sirro .

Kaskazini mwa Msumbiji katika Jimbo la Cabo Delgado, kumekuwapo na taarifa za kikundi cha kigaidi ambacho kinafanya uharifu kwa wakazi wa eneo hilo ambalo ni karibu na eneo la Kitaya, Mtwara.

Mei, mwaka huu, serikali ya Tanzania ilipeleka vikosi vya kijeshi mpakani mwa Msumbiji kama kuchukua tahadhari kufuatia mashambulizi ya kiuharifu yaliyokuwa yanafanywa na wanamgambo wa kikundi hicho ikiwamo uporaji, kuchoma makazi na mauaji kwa raia.

Ripoti ya BBC iliyotolewa Juni 3, mwaka huu, ilinukuu taarifa kutoka serikali ya Msumbiji kuwa kikosi cha ulinzi nchini humo kimewaua viongozi wawili wa kundi hilo ambao ni raia wa Watanzania, baada ya kuwapo kwa majibizano ya risasi katika Mkoa wa Cabo Delgado.

Kikundi hicho cha kigaidi kimekuwapo nchini Msumbiji tangu mwaka 2017 na inasadikiwa ni wafuasi wa kundi la dola ya Kiislamu (Islamic State) na pia kikundi hicho kimejipatia wafuasi kutoka Tanzania, Kenya, Rwanda na Burundi.

Wakati huo huo, IGP Sirro alisema tathimini inaonyesha kuwa, uchaguzi mkuu ulifanyika kwa amani isipokuwa kulikuwa na matukio ya watu watatu kuuwaa akiwamo askari polisi mmoja kuchinjwa na watu wasiojulikana.

Alisema kumekuwa na matukio mbalimbali ya kiuhalifu wakati wa kampeni na uchagauzi ambayo yalikuwa yanafanywa na baadhi ya wafuasi wa vyama vya upinzani na kuongeza kuwa jeshi hilo linawashikilia baadhi ambao walikuwa na lengo la kuvuruga amani.




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Simon Sirro, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu hali ya amani tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu hapa nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bibi wa miaka 95 auawa kwa kung'atwa na mbwa

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKAZI wa Mtaa wa Kimoro, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Tabia Kaniki (95), maarufu Bibi Londo, amefariki dunia baada ya kuvamiwa na kundi la mbwa na kumng`ata na wengine wawili kujeruhiwa sehemu mbalimbali za miili yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Jairy Khanga, alisema matukio hayo yalitokea katika nyakati tofauti.

Alisema Novemba 17, majira ya jioni kwenye Hospitali ya Serikali ya Mkoa wa Songea (HOMSO), alipokewa Tabia akiwa ameng`atwa sehemu mbalimbali za mwili wake na kupatiwa matibabu ya kutibu majeraha na tiba ya kinga, lakini baadaye alifariki dunia.

Dk. Khanga alisema, Novemba 14, mwaka huu majira ya mchana pia alipokewa Hadija Ally (23), mkazi wa Mpambalyoto, akiwa ameng`atwa sehemu mbalimbali za mwili hasa kwenye miguu na alipatiwa matibabu na baadaye aliruhusiwa kurudi nyumbani.

Alisema, Novemba 13, mwaka huu pia walimpokea Fabian Mathias (8), mkazi wa Mtaa wa Makambi akiwa na majeraha mengi mwilini ambaye kwa sasa hali yake bado si nzuri akiendelea kupata matibabu katika chumba cha maalumu cha uangalizi (ICU).

Ofisa Mifugo wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Deogratius Sibula, akiongea na waandishi wa habari alitoa rai kwa wananchi kuchukua tahadhari na kwa wenye mbwa kuwachanja.

Aliitaka jamii kuona umuhimu wa kuchukua tahadhari wanapowaona mbwa na wanao wamiliki wahakikishe wanawafunga minyororo na kuwafungia ndani.

Alisema serikali kupitia idara ya mifugo kwenye manispaa hiyo baada ya kupata malalamiko ya kuwapo makundi ya mbwa kudhurura mitaani na kuwavamia watu, wameshawaua mbwa 22 na operesheni hiyo inaendelea.

Pia alisema mwezi Mei, mwaka huu, walifanya operesheni ya kuwasaka mbwa wadhururaji na kufanikiwa kuwaua 151 katika mitaa ya Mpambalyoto, Msamala Machinjioni, Lizaboni Machinjioni na kwenye msitu wa Chandamali.

# TRA: Wasio na TIN namba kutolipwa mshahara Januari

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetangaza kuwa mfanyakazi ambaye hatawasilisha namba ya mlipa kodi (TIN number) hadi Desemba 31, mwaka huu hatalipwa mshahara wa Januari.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na chombo kimoja cha habari.

Kayombo alisema kila mfanyakazi anayelipwa mshahara anatakiwa kuwasilisha namba yake ya mlipakodi kwa mwajiri wake.

"Kila mwajiri anatakiwa kuwasilisha namba ya mlipakodi za waajiri wake kwenye malipo. Mchakato huu utakwisha Desemba 31, baada ya hapo mfanyakazi ambaye hatawasilisha, hatapata mshahara wa Januari, hii ni kwa wafanyakazi wote Tanzania," alisema.

Kayombo alifafanua kuwa mfanyakazi anapokatwa kodi katika mshahara wake, inatakiwa iende TRA ikionyesha kiasi kilichokatwa kwa mtumishi na namba ya mlipakodi.

"Lengo la kufanya hivi ni kwamba huu ndio utaratibu ambao unatumiwa duniani, tumechelewa kwa kuwa kila mlipakodi anatakiwa kulipa kwa TIN yake.

"Kilichokuwa kikileta utata kwa baadhi ya waajiri walikuwa wanasema wanalipa kodi nyingi, tukiwaomba watuletee hiyo kodi nyingi wanayolipa, wanaleta kodi ya mshahara ambayo siyo wao wanalipa bali mfanyakazi."

Alisema mabadiliko hayo yatasaidia kuondoa utata huo na kuainisha nani analipa kodi gani na itaonekana moja kwa moja.



Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo (kushoto), akizungumza na wafanyabiashara wa duka la vifaa vya magari, Aflah Habib (kulia) na Munin Habib, wakati akielimisha kuhusu kampeni ya elimu ya mlipakodi ijulikanayo Mlango kwa Mlango, katika Mtaa wa Lumumba, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Benki ya China yawekwa chini ya usimamizi wa BoT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeisimamisha Bodi ya Wakurugenzi na uongozi wa Benki ya Biashara ya China (China Commercial Bank Limited), huku ikichukua usimamizi baada ya kubainika kuwa na upungufu mkubwa wa mtaji.

Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Prof. Luoga alisema kwa mamlaka iliyopewa BoT chini ya kifungu cha sheria namba 56 (1) (g) (i) na (iii) cha sheria ya mabenki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, wameamua kuchukua usimamizi wa benki hiyo.

"Uamuzi huu umechukuliwa baada ya kubaini kuwa China Commercial Bank Limited, ina upungufu mkubwa wa mtaji, ukwasi wa kujiendesha yenyewe kinyume cha matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na kanuni zake," alisema Prof. Luoga.

Aidha, alisema upungufu huo wa mtaji unahatarisha usalama wa sekta ya fedha na pia kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa China Commercial Bank Limited, kutahatarisha amana za wateja wake.

Alisema, kutokana na uamuzi huo, BoT imeisimamisha Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi wa China Commercial Bank Limited.

Vile vile, alisema BoT, imemteua meneja msimamizi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za China Commercial Bank Limited, kwa kipindi ambacho itakuwa chini ya usimamizi wa BoT.

"Hivyo umma unaarifiwa kuwa katika kipindi kisichozidi siku 90, kuanzia siku ya taarifa hii, shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za China Commercial Bank zitasimama ili kuipa nafasi Benki Kuu ya Tanzania kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa suala hili," alisema Prof. Luoga.

Kadhalika, alisema hatua ambazo zinachukuliwa na BoT, ni kuhakikisha kuwa inatafuta njia ambazo zitaisaidia benki hiyo.

"Benki hii hatuifilisi ila tunachofanya ni kusimamisha shughuli zake kwa muda wa siku 90, ambazo BoT itakuwa imechukua usimizi wake chini ya mtu atakaye teuliwa kusimamia," alisema Gavana na kuongeza:

"Niwatoe hofu wananchi na kuwataka kuwa wavumilivu katika kipindi hichi cha siku 90 ambazo tutakuwa tumefunga huduma za benki hii."

Alifafanua kuwa benki hiyo inamilikiwa na wawekezaji kutoka China, na ilikuwa na tawi moja jijini Dar es Saalam.

# Simulizi mauaji ya bosi African Sports

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Klabu ya mpira wa miguu ya African Sports Club ya jijini Tanga, Abdul Ahmed maarufu Boznia, ameuawa kwa kupigwa na watu wanaodaiwa kuwa ni wafanya usafi barabarani.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa kipolisi wa Ilala, Janet Magomi, alilithibitishia Nipashe jana kuwa mauaji hayo yalitokea Jumatano eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam.

Naibu Ofisa Habari na Uhusiano SumaJKT, Kapteni Temilembe Kagaruki, akifafanua baadhi ya taarifa zilizosambaa mtandaoni juzi zilizodai waliotekeleza mauaji hayo ni vijana wa shirika hilo, alisema mpaka sasa hakuna uthibitisho wa ushiriki wa askari yeyote na wapo tayari kutoa ushirikiano kwa vyombo vingine vya ulinzi na usalama, ili kujua ukweli wake na wametoa pole kwa wafiwa.

Akisimulia kuhusu tukio hilo, Kamanda Magomi alisema Abdul alikuwa abiria kwenye pikipiki na wakiwa maeneo hayo, ghafla lilipita gari na kuwamwagia maji machafu yaliyotuama eneo hilo kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

"Baada ya tukio hilo, dereva wa bodaboda alikasirika na kulifukuzia hadi walipofika eneo mbele kidogo walilikuta na kulisimamisha na kumuhoji dereva aliyewamwagia maji machafu kwa nini amefanya hivyo," alisema.

"Kwa mujibu wa maelezo ya Abdul, kabla hajafariki dunia, kwenye gari kulikuwa na watu watatu ambao walikuwa na vifaa vya usafi yakiwamo mafagio, na walipowahoji ndipo hao watu walipoanza kumpiga na dereva wa bodaboda alipoona hivyo alikimbia," alisema.

Kamanda alisema Abdul alieleza baada ya kipigo walitokea wasamalia wema wakamchukua na kumpeleka kituo cha polisi cha Msimbazi ambako alipewa PF3 na kupelekwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Alisema siku tano mbele (Jumapili) alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu ya kutibu majeraha yake. Alisema katika tukio hilo alijeruhiwa mguu wa kulia na usoni na alikuwa akivuja damu.

Kamanda Magomi alisema mpaka jana hakuna mtu aliyeshikiliwa na wanaendelea kuwatafuta waliotekeleza mauaji hayo.

"Tayari tumeshapata taarifa kuwa waliosababisha kifo hiki ni wafanyakazi ambao wanafagia barabarani na halmashauri inawafahamu, tunawasaka popote walipo," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini, Ummy Mwalimu, katika ukurasa wake wa Instagram, aliandika jana kuwa, kifo chake kimekuwa cha ghafla na kimewaumiza hususani mazingira yaliyosababisha afariki dunia.

"Tumeumia sana, ninalaani tukio la kinyama alilofanyiwa nina imani kuwa vyombo vya dola vitafanya kazi yake," aliandika Ummy aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yafikisha kortini vigogo 3 BEVCO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewafikisha mahakamani vigogo watatu kati ya wanne wa Kampuni ya Vinywaji ya BEVCO LTD, kwa tuhuma za rushwa, ubadhirifu, utakatishaji wa fedha haramu na ukwepaji kodi zaidi ya Sh. bilioni 1.6.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhusiano wa Taasisi hiyo, Doreen Kapwani, watuhumiwa hao wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana.

Kapwani alibainisha kuwa kati ya watuhumiwa hao wawili ni raia wa Ufaransa na uchunguzi wa awali wa taasisi hiyo ulibaini tangu kusajiliwa kwa kampuni hiyo mwaka 2017 imekuwa ikichepusha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ambayo ilipaswa kulipwa serikalini.

Alisema fedha hiyo imekuwa ikiingizwa katika akaunti zao binafsi na kuisababishia serikali hasara.

Aliwataja watuhumiwa waliofikishwa mahakamani jana kuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Thierry Lefeuvre, Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni hiyo, Melanie Philippe, wote ni raia wa Ufaransa na Mwanasheria wa Kampuni hiyo, Ntemi Massanja.

Alitangaza donge nono la Sh. milioni 10 kwa atakayefanikisha kukamatwa meneja fedha wa kampuni hiyo, Joseph Samson.

"Uchunguzi wa TAKUKURU Makao Makuu umebaini watuhumiwa hawa wamehusika kwa kutenda makosa ya rushwa na uhujumu uchumi kwa kughushi nyaraka, kushindwa kulipa VAT, kutakatisha fedha haramu," alisema.

Alisema uchunguzi wa TAKUKURU bado unaendelea ili kubaini watuhumiwa wengine waliohusika kwenye tuhuma hizo pamoja na kiasi kingine cha fedha kilichohujumiwa.



Muuza chakula akipita kwenye tope katika soko la Mabibo jijini Dar es Salaam maarufu kama 'mahakama ya ndizi', kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania kinara kasi usajili vizazi kwa watoto Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA imechaguliwa na Umoja wa Afrika (AU) kuwa kati ya nchi tano za Afrika zitakazoongoza kampeni ya kuongeza kasi ya usajili wa vizazi kwa watoto.

Kampeni hiyo inayojulikana kama "Bila kuwa na Jina, Utambulisho wa Kisheria kwa kila mtoto, upatikanaji wa haki kwa kila mtoto, inaendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na AU.

Taarifa iliyotolewa na AU Novemba 3, 2020 ilieleza Tanzania itatekeleza jukumu hilo katika nchi za ukanda wa Mashariki wa Bara la Afrika na imechaguliwa kutokana na mafanikio iliyoyapata miaka ya karibuni katika kuongeza kasi ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu hasa usajili wa vizazi kwa watoto.

Ilisema sababu nyingine zilizoainishwa ni pamoja na nchi kuwa na utashi wa kisiasa katika masuala ya usajili wa vizazi na kutekeleza kikamilifu kanuni muhimu zinazounga mkono kampeni hii.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Emmy Hudson, ilisema kama nchi kiongozi, Tanzania inatakiwa kufanya kazi na Au katika kufanikisha kutangaza kampeni hiyo ndani ya nchi na katika Ukanda wa Mashariki ya Afrika na kuchukua taarifa za mafanikio na kuzitangaza katika hafla mbalimbali za kanda na Bara la Afrika.

Taarifa hiyo ilisema Tanzania pia inatakiwa kuwezesha nchi kubadilishana taarifa za mafanikio, kusaidia masuala ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu hasa usajili wa vizazi kuwa ajenda ya Umoja wa Afrika, kushiriki katika kutafuta raslimali fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo kwa ajili kuendesha masuala ya usajili wa vizazi katika ngazi ya Kanda na Bara la Afrika.

"Kampeni hii ilizinduliwa mwezi Juni 2020 kwa lengo la kuhakikisha kila mtoto anatambuliwa katika mifumo rasmi ya serikali kwa ajili ya kumwezesha kupata haki mbalimbali na usajili wa kizazi ni jambo la msingi katika kufikia hatua hiyo," ilisema.

Uzinduzi wa kampeni hiyo umekuja katika wakati sahihi huku wasiwasi ukiongezeka juu ya kushuka kwa viwango vya usajili wa vizazi kutokana na uwepo wa janga la (COVID-19)," ilisema taarifa hiyo," iliongeza.

Vilevile, ilisema kama nchi kiongozi, Tanzania ilipewa nafasi ya kuwasilisha mada katika kikao cha mawaziri na viongozi wa ngazi za juu wa nchi za Afrika kuhusu masuala ya usajili wa vizazi ambapo kauli mbiu ya kikao ilikuwa "Kuelekea usajili wa vizazi vyote Barani Afrika; Changamoto na fursa katika kipindi cha ugonjwa wa COVID-19".

**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI**

**(RITA)**

## TAARIFA KWA UMMA

### TANZANIA YANG'ARA NA KUCHAGULIWA NA UMOJA WA AFRIKA KUONGOZA KAMPENI YA KONGEZA KASI USAJILI WA VIZAZI KWA WATOTO BARANI AFRIKA

Tanzania imechaguliwa na Umoja wa Afrika (AU) kuwa kati ya nchi tano (5) za Bara la Afrika zitakazoongoza Kampeni ya kuongeza kasi ya Usajili wa Vizazi kwa Watoto Barani Afrika inayojulikana kama **"Bila kuwa na Jina; Utambulisho wa Kisheria kwa kila mtoto; Upatikanaji wa haki kwa kila mtoto"** ambayo inaendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Umoja wa Afrika (AU).

Taarifa iliyotolewa na Umoja wa Afrika tarehe Novemba 3, 2020 inaeleza kwamba Tanzania itatekeleza jukumu hilo katika nchi za ukanda wa Mashariki wa Bara la Afrika na imechaguliwa kutokana na mafanikio iliyoyapata miaka ya karibuni katika kuongeza kasi ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu hasa usajili wa vizazi kwa watoto. Sababu nyingine zilizoainishwa ni pamoja na nchi kuwa na utashi wa kisiasa katika masuala ya usajili wa vizazi na kutekeleza kikamilifu kanuni muhimu zinazounga mkono kampeni hii.

Kama nchi kiongozi, Tanzania inatakiwa kufanya kazi na Umoja wa Afrika katika kufanikisha mambo yafuatayo:

- Kuitangaza kampeni hii ndani ya nchi na katika Ukanda wa Mashariki ya Afrika
- Kuchukua taarifa za mafanikio na kuzitangaza katika hafla mbalimbali za kanda na Bara la Afrika
- Kuwezesha nchi kubadilishana taarifa za mafanikio
- Kusaidia masuala ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu hasa Usajili wa Vizazi kuwa ajenda ya Umoja wa Afrika
- Kushiriki katika kutafuta rasilimali fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo kwa ajili kuendesha masuala ya Usajili wa vizazi katika ngazi ya Kanda na Bara zima la Afrika.

Kampeni hii ilizinduliwa mwezi Juni 2020 kwa lengo la kuhakikisha kila mtoto anatambuliwa katika mifumo rasmi ya Serikali ili kumwezesha kupata haki mbalimbali na usajili wa kizazi ni jambo la msingi katika kufikia hatua hiyo. Uzinduzi wa kampeni hiyo umekuja katika wakati sahihi huku wasiwasi ukiongezeka juu ya kushuka kwa viwango vya usajili wa vizazi kutokana na uwepo wa Janga la Homa Kali ya Mapafu (COVID-19). Vilevile, kama nchi kiongozi, Tanzania ilipewa nafasi ya kuwasilisha mada katika Kikao cha Mawaziri na Viongozi wa ngazi za juu wa nchi za Afrika kuhusu masuala ya Usajili wa Vizazi ambapo kauli mbiu ya kikao ilikuwa **"Kuelekea Usajili wa Vizazi vyote Barani Afrika; Changamoto na fursa katika kipindi cha ugonjwa wa COVID-19".** Maamuzi mazuri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli katika kupambana na Covid-19 yaliwezesha huduma za usajili wa vizazi kuendelea kama kawaida kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya mfano katika Bara la Afrika.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Tanzania imefanya maboresho makubwa katika mfumo wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu hasa Usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto walio na Umri Chini ya Miaka Mitano (Under-Five Birth Registration Initiative) katika kutekeleza miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama Malengo Endelevu ambapo Lengo la 16.9 linataka nchi wanachama kutoa utambulisho kisheria kwa watu wote ikiwemo usajili wa vizazi ifikapo Mwaka 2030, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Ilani ya Chama Tawala - Chama cha Mapinduzi (CCM) .

Mpango wa Usajili wa Watoto Walio na Umri wa Chini ya Miaka Mitano mpaka sasa unatekelezwa katika Mikoa 18 umewezesha kugatua majukumu ya usajili na kusogeza huduma hiyo karibu na makazi ya wananchi ambapo zaidi ya watoto Milioni 5.2 wameweza kusajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa hivyo kuongeza kiwango cha usajili ya watoto wa kundi hilo kutoka asilimia 13 Mwaka 2012 mpaka kufikia asilimia 49.4 Mwaka 2020. Utekelezaji katika mikoa 8 iliyobaki unatarajiwa kukamilika Mwaka 2022.Mpango huu unatekelezwa kwa Ushirikiano na UNICEF, Serikali ya Canada na Kampuni ya simu ya TIGO.

Tanzania kama nchi nyingine barani Afrika, inapimwa katika utekelezaji wa Lengo Na.16.9 ya Malengo Endelevu (Sustainable Development Goals) kuhusu utambuzi wa watu ikiwemo usajili wa vizazi. Usajili wa vizazi ni nyenzo muhimu katika upatikanaji wa haki na huduma mbalimbali kwa mtu mmoja mmoja ikiwemo haki ya kutambulika, kurithi na kupata huduma za elimu na afya. Vile vile, Serikali kupitia Mfumo wa Usajili inapata taarifa za wananchi na takwimu ambazo ni za msingi katika utambuzi na kupanga mipango ya maendeleo ya nchi katika kusimamia utawala bora na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kama taasisi ya Serikali iliyopewa jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya Usajili nchini tunaahidi kushirikiana na kila mdau kuhakikisha kwamba kama nchi tunalitekeleza jukumu hili kikamilifu.

**Emmy K. Hudson**
**Kaimu Kabidi Wasii Mkuu/ Afisa Mtendaji Mkuu**
**19 Novemba, 2020**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bado kuna kazi kubwa kumaliza ukatili kijinsia

**MAADHIMISHO** ya Siku 16 za Kupinga Ukatili yanaanza Novemba 25 hadi Desemba 10, kwa kauli mbiu ya Maendeleo ya Mwanamke ni Faida kwa Jamii nzima.

Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ni kampeni ya kimataifa inayoongozwa na kituo cha kimataifa cha wanawake katika uongozi tangu mwaka 1991.

Chimbuko la siku 16 za kupinga unyanyasaji wa kijinsia ni mauaji ya kinyama ya kina dada wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominica mwaka 1960.

Mwaka 1991 Umoja wa Mataifa (UN) ulichagua Novemba 25 iwe siku ya kimataifa ya kupinga ukatili wa kijinsia na kilele chake ni Desemba 10, ya kila mwaka.

Maadhimisho haya hutoa mwanga wa uelewa kwa jamii kwa siku nyingine muhimu kama Novemba 29 Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Wanawake, Desemba 1, Siku ya Ukimwi Duniani, Desemba 6 Siku ya Mauaji ya Kikatili ya Montreal 1989 (wanawake 14 waliuawa na mtu aliyekuwa anawachukia wanawake) na Desemba 10 Siku ya Haki za Binadamu Duniani.

Lengo la maadhimisho haya ni kutoa fursa kwa wanawake, wanaume, vijana wa kike na kiume na wanaharakati wengine kukuza uelewa wa umma ya mchango wa wanawake katika maendeleo na kutafakari matokeo ya harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi.

Maadhimisho haya yanafanyika wakati ambao Tanzania kuna ongezeko kubwa la matukio ya ukatili wa jinsia dhidi ya watoto na wanawake, mchango wa mwanamke unazidi kudidimia kwa kuwa sasa anashambuliwa na baadhi ya wanajamii kiasi cha kumuumiza kisaikolojia.

Jitihada nyingi zimefanywa na mashirika ya kutetea haki, usawa wa kijinsia na ulinzi dhidi ya makundi yaliyo pembezoni hasa wanawake na watoto, ambayo kwa sasa yanaadhimisha siku hii kwa visa na mkasa, kutoa shuhuda hadharani, ikiwamo kushirikiana na mamlaka za kiserikali na dola katika kuunganisha nguvu kutokomeza kabisa ukatili wa kijinsia.

Kwa sasa ni imekuwa kawaida kila siku kuwapo tukio la ukatili wa kijinsia kama mwanamume kumshambulia mkewe kwa silaha ya jadi na moto na kusababisha ulemavu, kifo kwa kisingizio cha wivu wa mapenzi.

Pia, matukio ya watoto kulawitiwa na kubakwa ni mengi kwa mfano, hivi karibuni yameripotiwa katika mikoa ya Katavi, Morogoro, Dar es Saalam, Arusha, Lindi na Mtwara, jambo linadhihirisha bado kuna kazi kubwa inapaswa kufanywa ili kusaidia kizazi kinachoharibiwa sasa.

Kadhalika, kuna matukio yameripotiwa hivi karibuni katika maeneo kadhaa, yakiwamo ya watu kadhaa kuwafanyia vitendo vya ulawiti watoto wa ndugu zao.

Hali hii inashangaza na kuacha maswali mengi kwamba kwa nini wanaamua kufanya hivyo bila kujali kuwa ni kinyume cha sheria ha haki za binadamu?

Siku hizi vyombo vya habari vinaripoti matukio haya na ya wanawake kuuawa au kukatwa viungo.


Matukio haya yanashtua na kujiuliza imani ya dini iko wapi, utu umepotea miongoni mwa watu kwa kiasi gani cha kuharibu watoto kiasi hiki, anayeharibu watoto hivi kama naye angeharibiwa tungekuwa na kizazi cha sasa, wapi jamii inaelekea ikiwa watoto wataharibiwa kiasi hiki na mwisho tutapungukiwa baba wa baadaye.

Matukio haya yanatuma ujumbe wa viongozi wa dini kwama bado kuna jambo la kushughulikia kiimani, ili watu wawe na hofu ya Mungu na kutotenda matukio haya.

Tunashauri viongozi wa dini waongeze bidii katika kufundisha, kuwafikia waumini hadi maeneo yao ya makazi. Bila kuisaidia jamii matukio mabaya yanaongezeka na ambayo hayamfurahishi Mungu kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Ptotace

# Wajasiriamali mboga mjali afya za wateja wenu jamani!

**NI** msimu wa mvua. Kila mahali hasa kwa wakazi wa mikoa ya Pwani kuna msamiati mvua, ukizidi kupanuka katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Ni mvua na hata simulizi ya mafuriko, huku barabara zimeharibika, kule kilio cha madaraja, ili mradi majanga tu.

Wadau wakuu wa hali ya hewa wiki iliyopita, wanatudokeza kwamba na tusishangae, likawapo kwa wiki zaidi. Mafuriko hayo yanatokana na maendelezo ya mvua zinaendelea kuonyesha hivi sasa.

Kuna tahadhari zinazotolewa kwa kila mtu anao wajibu wa kuchukuwa hatua za kujihami hata kupata shida zitokanazo na athari zake. Hapo ni mimi na wewe ndio tunaotakiwa kuchukua hatua na kamwe sio mtu mwingine kwa niaba yako. Kuwa sehemu tu mapambano.

Jamii kutokana na mvua zinazonyesha, watu wanatakiwa kuzingatia masuala ya usafi na kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Hapo niseme kuna baadhi ya watu wasiowapenda wenzao au kutowatakia neema katika kipindi hiki cha mvua wanakitumia kutapisha 'chemba' za vyoo vyao na kuzuia tafrani ya kiafya, huku wakijua wazi kufanya hivyo ni kosa kisheria na hata kijamii.

Kanuni na sheria zote tunazifahamu na mamlaka zetu, hadi ngazi ya serikali za mitaa zinahimiza hilo. Sasa, kulikoni mtu anaona ni bora kutafuta watu wamzibulie ili awapatie pesa kidogo, badala ya kukodi gari la kutoa huduma ya kunyonya vyoo.

Hivi sasa, mtu anayefanya hivyo ajue hamtendei haki jirani yake na umma unaonzunguka na hata tafsiri na zaidi ya hapo.

**Hapo niseme kuna baadhi ya watu wasiowapenda wenzao au kutowatakia neema katika kipindi hiki cha mvua wanakitumia kutapisha 'chemba' za vyoo vyao na kuzuia tafrani ya kiafya, huku wakijua wazi kufanya hivyo ni kosa kisheria na hata kijamii.**

Ukija kwa wenzetu wanaouza matunda, mboga na bidhaa za aina mbalimbali, nao wanajua vizuri kipindi hiki na namna wanavyotakiwa kuchukua tahadhari za kiafya.

Hapo unakuta mvua inanyesha, ikimpa ishara kwmba anahitaji kuhifadhi bidhaa zake kwa ubora. Tujiulize wanalitenda hilo? La hasha, hata kidogo!

Umma huo wa wajasiriamali wanaotulisha, wengi wanashindwa kabisa kutekeleza kigezo hicho muhimu katika ujasiriamali.

Ni jambo linalofanyika,wakiwa waelewa wazuri wa dhana kama maradhi ya tumbo, kuhara, kichocho na hata kilio cha kipindupindu.

Unakuta mtu anajua umuhimu wa kumjali mteja na kufanya hivyo, lakini hajengi mazingira rafiki katika namna ya kuuza, kama vile kuziosha.

Ukija kwenye vitafunwa, hapo ni kazi haviosheki na vilevile vimeachwa katika namna hatarishi. Wauzaji wanawaza pesa tu, ndio wanaowakimbilia.

Ndani ya mvua hizi, ndio wakati sahihi kwa wafanyabiashara kubuni mbinu sahihi za kujihami.

Bila kufanya hivyo, ni kujimaliza na mvua ni kitu kilicho endelevu, hakikwepeki, bali cha kupambana nacho.

Kinachotakiwa kikuu ni kujiongeza kama mvua itanyesha nini kinatakiwa kufanyika na sio kuendelea kutoa huduma katika maeneo na namna isiyofaa.

Jijini Dar es |Salaam, eneo la Mabibo, kuna soko la ndizi, biashara ikiwa imeshamiri na kuna matope mengi yamejaa mahali hapo.

Mahali hapo kuna mengi zaidi ya mikungu ya ndizi imejaa kwenye matope, sambamba na bidhaa nyinginezo.

HABARI KITAIFA

# Ndikilo akumbana na uhaba wa saruji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amefanya ziara ya siku moja kwa wauzaji wa saruji katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha kukagua bei na kubaini hali halisi ya bei na upatikanaji wake.

Ndikilo katika ziara yake hiyo jana, alisema aliamua kufanya hivyo baada ya kudhani kwamba saruji haipatikani na ndiyo sababu ya kupanda kwa bei, lakini amepata picha halisi ya tatizo.

Katika ziara hiyo baadhi ya maduka yalikutwa hayana saruji kabisa huku mengine yakiwa na kiasi kidogo wengi wakilalamika foleni iliyopo viwandani.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema wauzaji wa saruji wa umoja huo wanategemea kupata bidhaa hiyo kutoka kiwanda cha Dangote, Simba na Camel, hivyo foleni inayoelezwa inawezekana kuwa chanzo cha kupanda kwa gharama za uuzaji.

Baadhi ya wauzaji wa bidhaa hiyo walilalamika mbele ya Ndikilo juu ya kutopatikana kwa bidhaa hiyo kwa wakati. Mchicha Mohamed alisema kwa sasa anauza saruji kwa Sh. 15,000 wakati awali bei ilikuwa Sh. 14,000 huku akinunua kwa Sh. 13,500.

Mchicha alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa kwa sasa upatikanaji wa saruji umekuwa wa shida kutokana na madereva kukaa kwa muda mrefu foleni ya kusubiri mzigo.

Naye Adam Mwasha alisema tangu Novemba 15 hadi sasa, hana saruji ya kuuza kutokana na foleni iliyoko katika kiwanda cha Simba huko Tanga huku Halfan Mwembamba akiongeza kuwa upatikanaji wa saruji umekuwa kikwazo kwao kufanya biashara vizuri pamoja na mabati ambayo nayo yameanza kuwa adimu.

Ofisa Masoko wa Wakala wa Usambazaji wa Saruji ya Kampuni ya Twiga, Denis Madege, alisema kiwanda chao kinaendelea na uzalishaji, lakini kutokana na mahitaji kuwa makubwa, upatikanaji wake umekuwa kikwazo.

Madege alisema wako watu walemilipia tani 300 za saruji, lakini hadi sasa hawajakamilisha oda hiyo kutokana na foleni iliyoko kiwandani.

Wauzaji waliotembelewa na mkuu huyo wa mkoa wanauza saruji mfuko mmoja kwa Sh. 14,700, Sh. 15,000 na Sh. 15,500.

# Dodoma yashika mkia ujenzi vyoo bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetaja mikoa mitatu inayosuasua kwenye ujenzi na matumizi ya vyoo bora kuwa ni Dodoma, Kigoma na Lindi.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Subi, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maadhimisho ya Siku ya Matumizi ya Choo Duniani ambayo hufanyika Novemba 19, kila mwaka.

Alisema mbali na mikoa hiyo pia baadhi ya mikoa ya Kanda ya Ziwa inasuasua kwenye ujenzi na matumizi ya vyoo hivyo huku akitaja mikoa vinara wa vyoo bora kuwa ni Dar es Salaam, Iringa na Njombe.

Dk.Subi akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, aliwataka watendaji kuanzia ngazi za mashina kuhamasisha ujenzi wa vyoo na kuhakikisha kila mwananchi anatumia choo bora.

"Tuhamasishe jamii kuhusu matumizi ya vyoo bora ili kujikinga dhidi ya maradhi ya kuambukiza yakiwemo ya kuhara, kuhara damu, kipindupindu na magonjwa ya minyoo," alisema.

Alifafanua kuwa choo bora kinapaswa kuwa na sakafu inayosafishika, ukuta, mlango, kilichoezekwa vizuri na chenye sehemu ya kupumilia ili kuondoa harufu ndani ya choo. Alisema matumizi ya vyoo bora ni afua muhimu katika kukinga na kudhibiti maradhi ya kuambukiza huku akisema asilimia 40 ya magonjwa yanayosababishwa na uchafu yanaepukika.

"Naagiza maofisa afya nchini kote kufanya ukaguzi katika maeneo ya shule, taasisi, kumbi za starehe, baa na maeneo yote yenye mikusanyiko kuangalia kama kuna vyoo vinavyokidhi vigezo," alisema.

Kadhalika, aliitaka jamii kuendelea kunawa mikono kwa maji safi na sabuni mara kwa mara ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Mratibu wa Programu ya Huduma Jumuishi za Kifedha katika Kuboresha Afya na Usafi wa Mazingira (FINISH MONDIAL), Christopher Ndangala, alisema programu hiyo imesaidia kuongeza ujenzi wa vyoo bora katika Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara kutoka asilimia ya 32 Julai 2018 hadi asilimia 50.71 mwaka huu.

"Mradi huu unatekelezwa kwenye kata 11 ambapo utekelezaji wake unafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kupitia Idara yake ya Afya na Mazingira, Shirika lisilo la kiserikali la AMREF na HACH, na imesaidia kuongezeka kwa vyoo bora vinavyojengwa kwa gharama nafuu,"alisema.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano wa mwaka wa Jumuiya za Asasi na Taasisi zinazojihusisha na usambazaji maji na usafi wa mazingira (ATAWAS) Jijini hapa, Ndangala alisema kuongezeka kwa ujenzi huo kumetokana na fursa ya mikopo ya ujenzi wa vyoo inayotolewa na taasisi za fedha ikiwamo Benki ya Equity ili kusaidia wananchi kuwa na vyoo bora.

"Kwa mfano Julai hadi Oktoba mwaka huu, vyoo bora 862 vimejengwa ambapo kati ya hivyo asilimia 32.71 vimejengwa kwa mikopo ambayo imetolewa na taasisi za fedha pamoja na benki ya Equity na kwa wastani wa mkopo unaotolewa ni Sh. 250,000 hadi Sh.600,000 kulingana na mahitaji ya kaya husika na uwezo wa kulipa,"alisema.

Aidha, alisema mradi huo umesaidia kuwajengea uwezo mafundi 35 wa kata 11 za wilaya hiyo na imekuwa ajira kwao ya kusaidia ujenzi wa vyoo bora.



Ofisa Programu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jackson Malangalila, akizungumza wakati wa semina iliyoshirikisha watu wa kada mbalimbali kwa lengo la kutambua umuhimu wa jinsia na maendeleo, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mmiliki wa shule Dar ashikiliwa na polisi

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Mkoa wa kipolisi Ilala, Dar es Salaam, linamshikilia Atuganile Mbosolelo, mmiliki wa Joy Unit Day Care, akituhumiwa kumiliki shule bila kibali.

Juzi, shule hiyo iliyoko Mtaa wa Kisiwani, Kata ya Bonyokwa, Segerea, ilidondokewa na ukuta wa nyumba ya jirani na kusababisha vifo vya watoto watatu na sita kujeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ilala, Janeth Magoni, alisema wamebaini mmiliki huyo anatoa huduma hiyo ya elimu bila kufuata kanuni na taratibu ikiwamo kibali.

"Mmiliki tunaye yule mama (Atuganile), tunamshikilia kwa sababu lazima tumshikilie shule yake haina kibali haitambuliwi. Shule aliyoitengeneza mwenywe ina wanafunzi 16, lakini tunaendelea kumtafuta yule mwenye ukuta ulioangukia hilo jengo. Tumemtambua kwa jina moja la Majani na tunaendelea kumtafuta," alisema.

Juzi majira ya 3:00 asubuhi, kabla ya masomo kuanza, ghafla ukuta wa shule hiyo ulianguka baadhi ya watoto wakitoka nje ya darasa kwa mujibu wa Atuganile.

Alisema shule hiyo ya awali ambayo ina miaka mitatu, aliianzisha kutokana na kuwa na taaluma hiyo na uzoefu kwenye kazi kwa takribani miaka 10.

Mbunge wa Segerea, Bonnah Kamoli, kupitia ofisi yake, alisema amepokea kwa masikitiko taarifa za maafa yaliyotokea katika shule hiyo.

Alisema alimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, kwa kufika eneo la tukio.

"Sisi sote ni waja wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea Inshallah! Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi. Lakini kwa umoja wetu tuzielekeze dua zetu kwa Mwenyezi Mungu, awaponye majeruhi wote," alisema Kamoli.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa mwongozo wa hatua kadhaa ikiwamo kuthibitishwa kuwa mwenye shule na meneja wa shule, maombi ya kusajili shule na usajili wa walimu, kabla ya kabla ya kuanziasha shule, ambao umeeleza:

Pia inatakiwa kuwapo andiko la mradi la wizara, 'Bank Statement' yenye zaidi ya Sh. milioni 62, nakala ya hati au uthibitisho wa kumiliki ardhi iliyotolewa kwa matumizi ya shule inayotambulika kisheria na serikali kuu ya mtaa au kijiji (eneo lisipungue ekari saba na nusu kijijini na ekari tatu na nusu mjini.

Kadhalika, kunatakiwa kuwe na michoro ya majengo ya shule inayoonyesha vipimo kwa kuzingatia viwango vya wizara, ramani ya shule inayoonyesha mpangilio wa majengo na viwanja vya michezo, cheti cha usajili wa kampuni, shirika, umoja, asasi ya kiraia (NGO), iwapo shule ni ya jumuiya na katiba yake au mkataba wa maridhiano.

# GGML, NEEC wawezesha mafunzo w/biashara 500

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuwapatia maarifa na ujuzi wajasiriamali mkoani Geita juu ya mchakato wa manunuzi yanayofanywa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), kampuni hiyo imefadhili mafunzo maalum yanayoratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Mafunzo hayo ni matokeo ya makubaliano yaliyofikiwa na GGML na NEEC Julai 20, mwaka huu kuhusu namna bora ya kuwasaidia wajasiriamali mkoani Geita, ili wapate fursa bora ya kufanya biashara na taasisi mbalimbali nchini ikiwamo GGML.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mafunzo hayo mjini Geita, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson, alisema kampuni hiyo inalenga kuboresha ushiriki wa wafanyabiashara mkoani humo katika zabuni mbalimbali zinazotangazwa na kampuni hiyo.

Alisema malengo hayo ni kuwajengea uwezo, ili wafahamu vigezo muhimu na kutimiza matakwa ya kisheria kusambaza bidhaa na huduma mbalimbali kwenye sekta ya uchimbaji madini sambamba na sekta zingine.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo ni uthibitisho tosha kuwa GGML inakusudia kuchochea maendeleo endelevu kwa jamii inayozunguka mgodi.

"Tumeendelea kuthibitisha haya kwa vitendo kwa kushirikiana na serikali kuboresha huduma za kijamii ikiwamo elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara pamoja na shughuli mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi maeneo yanayozunguka mgodi," alisema Jordinson.

Alisema mpango huo unaotumia bajeti ya shilingi bilioni 1.3 za Kitanzania, unawalenga wajasiriamali 500 wanaoishi mkoani Geita wakiwamo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017, GGML kupitia fedha za uwajibikaji wa kampuni kwa jamii imeshirikiana vyema na halmashauri mkoani Geita kutekeleza miradi ya maendeleo kwa jamii yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 30 mkoani Geita," alisema Jordinson.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji NEEC, Beng'i Issa, aliipongeza GGML kwa mpango huo ambao unaendana na mpango wa kuendeleza biashara mkoani humo.

"Mpango huu utawajengea uwezo na kujiamini wajasiriamali na kushindana vyema na wafanyabiashara wengine nchini ili baadaye waweze kuboresha mapato na maisha yao," alisema Beng'i Issa.




Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa akizungumza na washiriki wa mafunzo ya wafanyabiashara mkoa wa Geita jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaweka nguvu utafiti uvuvi

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, amesema serikali imeweka nguvu katika masuala ya utafiti kwenye sekta ya uvuvi nchini, ili kuhakikisha inapata taarifa sahihi ya maeneo ya uvuvi, kuzalisha vifaranga bora na chakula bora cha samaki.

Dk. Tamatamah alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa maabara ya kisasa ya utafiti wa uvuvi itakayotumika na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

Maabara hiyo inaengwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH).

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wa masharti nafuu wa Sh. bilioni 2.6, unalenga kukuza sekta ya uvuvi nchini.

"Katika uchumi wa bluu katika awamu hii tunategemea meli nane kwenye uvuvi wa bahari kuu, hivyo ni lazima watafiti kama TAFIRI waende baharini. Pia tuna mpango wa kuongeza uzalishaji wa samaki kupitia ufugaji kwenye maeneo mawili ya chakula bora na vifaranga bora, hivyo utafiti ni muhimu kupitia maabara hii," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema katika miaka mitano ijayo serikali imepanga kupunguza matatizo ya upatikanaji wa vifaranga vya samaki na chakula bora cha samaki hao.

Alisema mahitaji ya vifaranga ni milioni 50 kwa mwaka, lakini kwa sasa vifaranga vinavyozalishwa hapa nchini ni milioni 30 pekee.

Mratibu wa SWIOFISH Tanzania Bara, Nicholas Mlalila, alisema baada ya kukamilika kwa jengo hilo wataalamu watajikita katika kufanya utafiti na kwamba kwa sampuli za mazao ya samaki zimekuwa zikisafirishwa kwenda nje ya nchi kwa ajili ya utafiti.

Mlalila alisema serikali inatarajia kujenga maabara nyingine kupitia mradi huo kwa ajili ya kuzalisha vifaranga bora vya samaki wa baharini pamoja na mbegu za mwani katika kukuza sekta ya uvuvi.

Mkurugenzi Mkuu wa TAFIRI, Dk. Ismael Kimirei, alisema taasisi hiyo ina mikakati mingi katika kukuza utafiti wa uvuvi nchini kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kupunguza gharama za kutuma sampuli za uvuvi kwenda nje na hivyo sampuli zote kufanyiwa kazi katika maabara hiyo.

# Zimamoto yataka vipaumbele bajeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limetaja vipaumbele vyake katika bajeti ya mwaka 2020/21 ikiwamo upatikanaji wa vitendea kazi ili kurahisisha utoaji huduma na kukabiliana na majanga.

Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, John Masunga, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua baraza dogo la wafanyakazi wa jeshi hilo, lililofanyika jijini hapa.

Alisema moja ya agenda ambazo zitajadiliwa katika baraza hilo ni kupitia bajeti iliopo na ijayo ili kuboresha utendaji kazi.

"Hili jeshi kazi yake si ya majanga ya moto pekee, tunahusika hata na majanga mengine na linatoa huduma nyingi za uokoaji na si za moto pekee hivyo wananchi wanapaswa kutoa taarifa kwa haraka pale wanapoona kuna majanga yametokea," alisema.

Pia alisema tayari wameanzisha vituo 38 katika wilaya mbalimbali ambavyo vinasaidia katika utendaji kazi wao.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kwenda na kasi ya ukuaji wa miji, hivyo nao wanaendelea na ufunguaji wa vituo hivyo ili kuwarahisishia katika utendaji kazi.

Naye Mkurugenzi wa Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Emmanuel Kayuni, aliwataka wajumbe wa baraza hilo, kuondoka na ujumbe wenye majibu badala ya malalamiko ili kwenda kuboresha maeneo yao ya kazi.

Kayuni alisema wakiwa wawakilishi kutoka mikoa tofauti, wanapaswa kutumia ipasavyo baraza hilo kudai maslahi ya wafanyakazi wenzao.

Kadhalika, aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuwa makini kusikiliza agenda ambazo zitajadiliwa ndani ya baraza hilo.

"Baraza la wafanyakazi ni muhimu sana katika sehemu ya kazi, hivyo nyie wajumbe wawakilishi mnapaswa kubeba ujumbe wenye majibu ya kutatua kero mlizonazo badala ya kuondoka na ujumbe wa malalamiko unaokwenda kubomoa," alisema Kayuni.

**Lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kwenda na kasi ya ukuaji wa miji, hivyo nao wanaendelea na ufunguaji wa vituo hivyo ili kuwarahisishia katika utendaji kazi.**

# Waathirika kesi za udhalilishaji watakiwa kuhudhuria kortini

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAATHIRIKA wa kesi za udhalilishaji kisiwani Pemba wametakiwa kuwa tayari kufuatilia na kutoa ushahidi endapo kesi hizo zitafikishwa mahakaani.

Kauli hiyo imetolewa na Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) ofisi ya Pemba, Fathiya Mussa Said, wakati akizungumza na wazazi ambao watoto wao wamefanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Alisema kutokana na matukio hayo kutendeka katika jamii, ipo haja kwa wazazi kuwa mstari wa mbele kufuatilia na kutoa ushahidi wa kweli wanapoitwa mahakamani, jambo ambalo litasaidia wahalifu kutiwa hatiani.

"Tusipotoshe ushahidi maana tunamfanya mtendaji kosa asipate hatia, hii itasaidia wengine kuogopa kuwafanyia watoto ukatili," alisema mratibu huyo.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuwawezesha na kuwajengea uwezo waathirika wa matukio ya dhalilishaji, ili wasiwe na hofu ya kufuatilia na kutoa ushahidi.

"Kuna baadhi yao wanaogopa ile mahakama, kesi wanaipeleka polisi, lakini wakiitwa mahakamani kutoa ushahidi wanakimbia, hali hii hatuwezi kuondosha matendo haya, tushirikiane ili kukomesha," alisema.

Aliwataka wasimamizi wa kesi hizo wawatoe hofu waathirika hao wakati kesi zao zinapopelekwa mahakamni, kwani ndio sehemu pekee zinapopatikana haki zao.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Seif Mohd Khamis, alisema kuna baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kutowasikiliza na kutoyatilia maanani yale wanayoambiwa na watoto wao, jambo ambalo linasababisha kuendelea kufanyiwa udhalilishaji kwani wanaona ni hali ya kawaida.

"Kutokana na kujali shughuli zao kuliko watoto wao, watoto wanapowaripoti mapema wazazi wao, lakini huwapuuza, hivyo wanaona ni jambo la kawaida na hatimaye wanaendelea kudhalilishwa," alisema.

Alisema kuwa, kuripoti mapema ndio njia inayosaidia kwa kiasi kikubwa kupatikana ushahidi kwa wapelelezi, hivyo wazazi wajitahidi kuwasikiliza watoto wanapowashtakia kutendewa vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

Aidha, alisema ushahidi ndio kitu muhimu katika kuthibitisha jambo lolote ambalo lipo mahakamani, ingawa watoto wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 17 wanashindwa kutoa ushahidi, hivyo kusababisha kutohukumiwa.

Nao waathirika walisema, mara nyingi wanashindwa kufika mahakamani kutokana na kesi kukaa muda mrefu bila kutolewa hukumu na kushindwa kufuatilia.

Mkutano huo wa siku moja wa kuwajengea uwezo waathirika wa kesi za udhalilishaji, ulifanyika katika Ofisi ya TAMWA Chakechake Pemba.

# 'Vifo vya watoto wachanga bado tatizo'

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema vifo vya watoto wachanga ikiwamo njiti, bado ni tatizo kubwa, huku vikichangia asilimia 40 ya vifo vyote vya watoto walio chini ya miaka mitano.

Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu Mkuu wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Prof. Andrea Pembe, kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto Njiti Duniani, inayoadhimishwa kila Novemba 17.

Akisoma hotuba hiyo, Prof. Pembe alisema takwimu za mwaka 2015 na 2016 zinaonyesha, kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa hai watoto 25, hupoteza maisha kabla ya kutimiza siku 28.

"Vifo hivi vinachangia kwa takribani asilimia 40 ya vifo vyote vya watoto chini ya miaka mitano kwa takwimu za TDHS mwaka 2015 na 2016, vinavyotokea hapa nchini.

Taarifa za wizara zinaonyesha kuwa mwaka 2018 jumla ya vifo vya watoto wachanga 11,524 vilitolewa taarifa na mwaka 2019 jumla ilikuwa 9,681," alisema Prof. Pembe.

**Takwimu zinaonyesha watoto wachanga ambao wanafariki, ni kutokana na matatizo yanayoambatana na kuzaliwa na uzito pungufu hususan waliozaliwa kabla ya wakati.**

Alisema takwimu zinaonyesha watoto wachanga ambao wanafariki, ni kutokana na matatizo yanayoambatana na kuzaliwa na uzito pungufu hususan waliozaliwa kabla ya wakati.

"Mtoto kuzaliwa kabla ya wakati 'premature' ni kabla ya mimba kukamilisha wiki 37 za ujauzito. Hapa nchini tatizo hili ni kubwa, Taarifa ya 'World Population Prospects' ya mwaka 2013 inaonyesha Tanzania ni kati ya nchi 20 duniani zinazoongoza kwa kuzaliwa watoto njiti wanaofikia watoto 213,500 kwa mwaka," alisema Prof. Pembe.

Pia alieleza kwamba, watoto milioni 15 huzaliwa kila mwaka duniani wakiwa njiti na kuwa katika hatari ya kufariki kwa sababu ya kushindwa kutunza joto mwilini. Kupumua kwa tabu, kupata maambukizi ya bakteria na hata kuwa katika viungo vyao.

Meneja kitengo cha kujitolea kwenye Jamii Vodacom, Sandra Oswald, alisema kwa miaka mitatu wamedhamiria kuwekeza kupunguza vifo cha watoto wachanga, huku ikichangia Sh. milioni 100 na wamewafikia wanawake 8,000 nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Doris Mollel Foundation (DMF), inayojishughulisha kusaidia watoto njiti, Doris Mollel alisema lengo la maadhimisho ni kukumbuka watoto hao ambao kati ya milioni 15 wanaozaliwa duniani milioni moja hupoteza maisha duniani.

Bingwa wa Watoto Wachanga kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Augustine Massawe, alisema mwezi huu umelenga kuhamasisha umma kuhusu watoto hao, na kwamba mkoa wa Dar es Salaam pekee huzaliwa watoto njiti 2,000 kati ya watoto robo milioni wanaozaliwa nchini kila mwaka. Katibu Mkuu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, alisema serikali, itahakikisha inaendelea kuimarisha afya ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati, kwa kuwa na vyumba maalum katika hospitali.

"Maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na DMF, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kampuni ya simu ya Vodacom na benki ya NCBA, kauli mbiu ya mwaka huu ni 'pamoja na watoto wanaozaliwa kabla ya wakati kujali kesho yao'.



Meneja wa Ruzuku na Mawasiliano wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald (kushoto), akipata maelezo ya jinsi vifaa vya kuwasaidia watoto waliozaliwa kabla ya wakati (Njiti), vinavyofanya kazi kutoka kwa Mkunga Godlove Itungi (kulia), wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto Njiti Duniani, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Katikati ni Mtendaji Msaidizi wa KAS Medics, Flora Matthew. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi kujaribu kumuua mke yaahirishwa

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

KESI ya kujaribu kumuua mkewe na kumkata kiganja cha mkono kwa madai ya wivu wa mapenzi, inayomkabili mfanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Ombeni Alfayo (33), imepigwa kalenda hadi Desemba 2, mwaka huu.

Alfayo alifikishwa kwa mara ya kwanza katika Mahakama ya Wilaya ya Arumeru iliyoko Sekei mkoani Arusha, Novemba 4, mwaka huu.

Jana, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Christina Chitanda, anayesikiliza shauri hilo namba 19 la mwaka 2020, aliahirisha kesi hiyo baada ya upande wa mashtaka kuieleza mahakama kuwa bado upelelezi haujakamilika. Mshtakiwa Alfayo anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 196 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Mapitio mwaka 2002.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Chitanda alisema mshtakiwa Alfayo atarejea mahabusu katika Gereza Kuu la Kisongo hadi hapo kesi yake itakapotajwa tena mahakamani hapo.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo Septemba 26, mwaka huu, kwa kujaribu kumuua mkewe, Veronica Kidemi (30) ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiranyi na mkazi wa Kijiji cha Siwandeti, Wilaya ya Arumeru, na kumkata kiganja cha mkono wa kulia.

Katika tukio hilo, Alfayo alimkata mkewe kiganja cha mkono wa kulia na kukitenganisha na sehemu nyingine ya mkono.

# Watakiwa kuwatambua wanaougua ‘Haemophilia’

Na Beatrice Shayo

SERIKALI imewataka wataalamu wa afya kuwatambua wagonjwa wenye Haemophilia (upungufu wa damu unaosababisha ulemavu), ili waweze kupatiwa matibabu wasipate ulemavu kwa kuwa mpaka sasa Tanzania ina wagonjwa 167 na wanaoumwa ni zaidi ya 6,000.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Magonjwa yasiyoambukizwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. James Kiolowe wakati akisoma hutuba ya Mganga Mkuu wa Serikali kwenye uzinduzi wa mradi wa kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma kwa watu wenye magonjwa ya damu Tanzania katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Alisema asilimia 97 ya watu wenye Haemophilia duniani hawajagundulika bado, kwa upande wa Tanzania hadi sasa wagonjwa hao waliotambulika na wanaoendelea na matibabu ni 167.

“Uanzishwaji wa mradi huu utasaidia upatikanaji wa vipimo katika hospitali za rufani na mikoa na tunaamini wagonjwa wengi watatambulika na wataanzishiwa tiba stahiki,” alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kwa idadi ya watu waliopo nchini, Tanzania inaweza kuwa na wagonjwa wa Haemophilia kati ya 6,000-12,000, na watoto 11,000 wenye ugonjwa wa selimundu huzaliwa kila mwaka.

**Ukiwa na haemophilia ukachomwa sindano unaweza kutokea uvimbe mkubwa na hata kupata ulemavu na endapo tatizo hilo lisipojulikana mapema unazidi kupata madhara zaidi kwani wenye ugonjwa huo huwa wanapata maumivu makali na damu nyingi kutoka.**

Kiolowe alifafanua kuwa mradi huo utasaidia kuongeza kasi katika upatikanaji wa takwimu za ugonjwa wa hemophilia, utasaidia kufanyika utafiti wa ugonjwa huu na pia utaharakisha uboreshaji wa huduma kwa wagonjwa hawa pamoja na kuwekea ugonjwa huo katika mpango mkakati wa magonjwa yasiyoambukiza (NDC) na hatimaye kuwa na mwongozo wa utoaji huduma (katika hospitali zote nchini).

“Mradi huu pia utahusisha ununuzi wa mashine za kupima magonjwa haya kwa hospitali za rufani, pamoja na kutoa mafunzo maalumu ya kufanya vipimo hivyo kwa wataalamu wa maabara, pia utasaidia manunuzi ya vifaa vya mazoezi tiba kwa wagonjwa hawa kwani ugonjwa huu wa hemophilia husababisha ulemavu wa viungo kama usipotibika mapema na kupata mazoezi tiba,” alisema.

“Mradi utafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na waandishi wa habari, kuhakikisha uelewa wa magonjwa haya unaongezeka nchini,” alisema.

Aidha, alisema serikali imekuwa ikiwezesha upatikanaji wa huduma za matibabu kwa magonjwa ya damu ambazo ni za kibingwa na za gharama kubwa.

Alisema serikali peke yake haiwezi kuzimudu na kuzifanya endelevu bila kushirikiana na wadau wa sekta ya afya pamoja na sekta binafsi.

Daktari wa Hospitali ya Taifa Muhimbili MNH, Dk. Stella Rwezaura, alisema ugonjwa wa haemophilia husababisha hutokwa na damu nyingi mwilini na kusababisha ulemavu na wengine hufariki.

“Ukiwa na haemophilia ukachomwa sindano unaweza kutokea uvimbe mkubwa na hata kupata ulemavu na endapo tatizo hilo lisipojulikana mapema unazidi kupata madhara zaidi kwani wenye ugonjwa huo huwa wanapata maumivu makali na damu nyingi kutoka,” alisema.

Alisema tatizo lililopo ni wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na ugonjwa huo, huku wengine wakienda kwa waganga wa kienyeji.

Dk. Rwezaura alisema kuna wanaopewa rufani ya kwenda Muhimbili ili wapatiwe matibabu zaidi, lakini wanashindwa kufika kutokana na hali duni waliyokuwa nayo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MHN, Prof. Lawrence Museru, alisema upatikanaji wa tiba stahiki dhidi ya ugonjwa huo ni tatizo.

Alisema mradi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwapo wa huduma ya uhakika kwa wakati na wananchi kuwa na uelewa ili wasiendelee kupata ulemavu.



Mtendaji wa Mtaa wa Maweni, Kata ya Mjimwema, Wilaya ya Kigamboni, Koela Magai (kushoto), akipokea vitabu vya kuchukua taarifa za malalamiko kutoka kwa Ofisa Uhusiano Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Joseph Mkonyi, wakati wa ufunguzi wa madawati ya kusikiliza malalamiko ya wateja wa maji, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waliozingirwa na maji watakiwa kuhama makazi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI ambao nyumba zao zimezingirwa na maji mkoani Shinyanga, wametakiwa kuhama makazi yao na kwenda kuishi maeneo ambayo ni salama, ili kuepuka kuangukiwa na nyumba hizo na kusababisha maafa.

Mratibu wa maafa mkoani Shinyanga, Pastory Mfoyi, alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe, namna walivyojipanga kukabiliana na maafa katika msimu huu wa mvua.

Alisema wananchi ambao nyumba zao zimeshazingirwa na maji hasa za tope, wanapaswa kuhama kwenye makazi hayo, ambapo maisha yao yapo hatarini kwa kuangukiwa na nyumba hizo, kutokana na kutokuwa imara na kushindwa kuhimili mvua.

“Mkoa wa Shinyanga tumeshajipanga kukabiliana na maafa kuanzia ngazi ya kijiji, nitoe tu wito kwa wananchi waache kujenga nyumba za tope tena kwenye mabonde na mikondo ya maji, bali wajenge nyumba imara na wapande miti ili kuzuia nyumba kuezuliwa na upepo wa mvua,” alisema Mfoyi.

“Sasa hivi kuna taarifa za baadhi ya nyumba za tope kuezuliwa na upepo na nyingine kuanguka sababu ya mvua, lakini hazijaleta madhara kwa wananchi zaidi ya kuharibu mali zao, na waomba tu wananchi wale ambao nyumba zao zipo kwenye hatari, wahame mapema kabla ya kuwaangukia ili kuokoa maisha yao,” aliongeza.

Katika hatua nyingine alitoa tahadhari kwa wananchi kuwa makini na magonjwa ya mlipuko katika msimu huu wa mvua, ambapo vyoo hujaa maji na kutiririsha kinyesi, hivyo kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Mmoja wa wakazi wa Shinyanga, Beatrice Gerald, anayeishi Mtaa wa Mwanoni Kata ya Ndembezi, ambaye nyumba yake ilizingirwa na maji, alisema licha ya kupewa tahadhari hiyo, serikali nayo inapaswa kuboresha miundombinu kwa kuchimba mitaro, kwa ajili ya kutiririsha maji kuyaelekeza kwenye madaraja.

**Wananchi ambao nyumba zao zimeshazingirwa na maji hasa za tope, wanapaswa kuhama kwenye makazi hayo, ambapo maisha yao yapo hatarini kwa kuangukiwa na nyumba hizo, kutokana na kutokuwa imara na kushindwa kuhimili mvua.**

# Wanaharakati watoa neno Siku 16 za Kupinga Ukatili

Na Yasmine Ptotace

KATIKA kuelekea maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili, jamii imetakiwa iwe na nguvu ya pamoja katika kukataa au kupinga ukatili.

Hayo yalisemwa na Anna Sangai, ofisa programu wa harakati za ujenzi wa nguvu za pamoja kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alipokuwa akitoa mada kwa washiriki wa GDSS.

Siku 16 za kupinga ukatili huanza kila mwaka Novemba 25 na kumalizika Desemba 10.

“Tutumie siku hizo kuelimisha wanajamii, kupinga ukatili katika maeneo tunayokaa,” alisema.

Aliongeza kuwa siku 16 za kupinga ukatili zinamaana kubwa kwa jamii, ambapo pamoja na kupinga ukatili, pia Desemba Mosi ni Siku ya Ukimwi Duniani na Desemba 10 ni Siku ya Haki za Binadamu.

Alisema kauli mbiu ya siku ya kupinga ukatili ni ‘tupinge ukatili wa kijinsia mabadiliko yaanze na mimi’.

Aliongeza kuwa kama ‘mabadiliko yaanze na mimi’, inatakiwa kila mwanajamii kukemea ukatili katika maeneo yanayomzunguka na kufanya hivyo ukatili unaweza kupungua au kuisha kabisa.

Aliongeza kuwa lengo la kampeni ni kuhakikisha jamii inakataa au kupinga ukatili.


Alisema mwaka 2018 /2025 ni mkakati wa kupinga ukatili dhidi ya watoto na wanawake.

“Serikali ilisema mpaka mwaka 2022 ukatili uwe umepungua kwa asilimia 50,” alisema.

Aliongeza kuwa malengo hayawezi kufikiwa kama jamii itakuwa na ushirikiano wa kutoa taarifa za matukio ya ukatili, ili wahusika wachukuliwe hatua, na jamii inatakiwa kutowafumbia macho watu wanaofanya ukatili.

Sada Akida, mmoja wa washiriki wa GDSS, alisema matukio ya ukatili yapo na kinachotakiwa jamii isiwafumbie macho wanaotenda matukio hayo.

Pia alisema ili kukomesha matukio hayo yasiendelee, sheria ikabadilishwe badala ya kutoa dhamana kwa waliotuhumiwa kufanya ukatili, wangewaacha mahabusu na wakikutwa na hatia wanyongwe.




Ukurasa 13

Mazingaombwe ya Giaboksi Mtambo wa Chuma!



Ukurasa 12

**Majibu yanayowahamisha wafugaji kutoka 'kusaka nyoka' hadi sayansi**

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 20, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Msomi wa ujasiriamali atoa dozi kinamama kupita tundu sindano

## ●Mtaji wao; elimu, ujuzi na hulka
## ●Marufuku kubadili lengo la mkopo

**Na Sabato Kasika**

UWEKEZAJI katika biashara ndogo za kati na kubwa, ni miongoni mwa fursa zinazoendelea kuchangamkiwa na wanawake, kwa kuwa wana mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii.

Kutokana na kutambua umuhimu wao katika jamii, ni budi waachane na mazoea ya zamani, ambayo haikuwa rahisi kwa mwanamke wa Kiafrika kushinda kwenye biashara yake siku nzima.

Bado kunatajwa kuwapo baadhi ya wanajamii udhaifu ka kwa namna moja au nyingine, unaosababisha washindwe kupiga hatua.

Mtaalamu wa biashara na Mhadhiri katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Mariam Tambwe, anaeleza katika mazungumzo yake na gazeti, akitaja sababu kadhaa zinazomkwamisha mwanamke katika biashara.

Mariam anasema, mwanamke kuingia kwenye biashara bila kufanya utafiti na kukopa fedha za biashara na kisha kuelekeza kwenye mambo mengine ni tatizo ambalo liko ndani ya uwezo wake.

"Kabla ya kufanya biashara fulani, ni lazima mtu afanye utafiti kwanza ili kujua kama inaweza kuwa endelevu, siyo kuibuka tu na kuuza viazi na kumbe haina soko kwenye eneo analofanyia," anasema Mariam.

Anafafanua kuwa chanzo kikuu cha mitaji duniani kote ni mikopo rasmi ya kibiashara, ila binafsi katika maono yake anashangaa anaposikia na kuona baadhi ya wanawake wanakopa fedha za biashara na kuzihamishia kwenye matumizi mengine.

"Wanawake wenye mtindo huo ni wale walio na tamaa ya kutaka kuwa na kila kitu, hata kama hawana uwezo wa kukinunua, wanalazimika kukopa fedha kwa kisingizio cha kufanyabiashara na kumbe sivyo," anasema.

Mtaalamu huyo wa biashara, anawataka wanawake wenye mtindo huo wabadilike, ili biashara zao ziweze kukua na kuwaletea maendeleo na kwamba, inapotokea wanaendekeza tamaa, daima hawawezi kufika mbali kibiashara.

**NJE YA UWEZO**

Anasema, kuna sababu zilizoko nje ya uwezo kwa wanawake, anataja kukosa ushirikiano kutoka katika familia zinazoua ufanisi wa kazi hiyo .

"Unaweza kukuta mwanamke ndiye anayetegemewa kwa shughuli zote nyumbani hata kama mume yupo, hali inayosababisha ashindwe kusimamia biashara zake vizuri," anasema.

Mariam, ambaye mbali na stadi ya biashara, ana taaluma ya ualimu, anaongeza ukosefu wa elimu ya biashara unasababisha baadhi yao wasijue kutunza fedha, taarifa za biashara, uandaaji na uboreshaji wa biashara na hata kutafuta wateja.



Mhadhiri wa Chuo cha Elimu ya Biashara, Mariam Tambwe, alipokuwa kwenye semina. **PICHA: MTANDAO.**

Anahimiza kuwa uboreshaji kipato cha familia na jamii kwa ujumla, unafanywa kwa kiasi kikubwa na kinamama na kwamba kundi hilo halina budi kusaidiwa na kubadilika kila inapowezekana.

"Wanawake wengi wamechangakia fursa za biashara mbalimbali, lakini baadhi yao wanakwamishwa na wengine wanajikwamisha wenyewe kutokana na mtindo wao wa maisha, hivyo wajikwamue na wakwamuliwe" anasema.

Anasema, wajasiriamalia wanatakiwa kuhakikisha wanaangalia biashara zao, wajue wanafanya kitu gani, na kikubwa zaidi ni kila mmoja kujitahidi kupata elimu ya biashara ili aweze kufikia kile anachokusudia.

"Maana yangu ni kwamba, umefika wakati sasa wanawake waelimike na wajue nini wanatakiwa kufanya ili wawe na mchango mkubwa tunapoelekea kwenye Tanzania ya viwanda," anasema.

**KUJIAMINI?**

Mariam anasema, kuna matatizo kadhaa yanayowakabili wanawake, ikiwamo adha ya kukerwa na dai la rushwa ya ngono kutoka kwa wateja na watu wanaowazunguka katika biashara zao, ikiwa sharti ka kuwawezesha biashara zao ziende vizuri.

"Hivyo ili kukabiliana na matatizo hayo, ni muhimu kujiamini, pia ni lazima mwanamke uwe na vitu vikubwa vitatu vya kukuwezesha kusonga mbele katika biashara yako ambavyo ni elimu, ujuzi na hulka," anasema.

Anafafanua kuwa, si lazima kuwa na sifa zote tatu, lakini walau mfanyabiashara awe nazo hata mbili, ili ujiite mjasiriamali na uweze kumudu matatizo yanayopatikana katika biashara.

Mtaaluma huyo, anaeleza kuwa wanawake kujiamini na kuwa wabunifu wa biashara, ni jambo muhimu, kwa vile ndiyo njia pekee itakayowatofautisha na wafanyabiashara wengine.

Anawashauri: "Watambue kuwa kama ni wazalishaji au waagizaji wa bidhaa waagize nyingi, isije mteja akaja na kuikosa, kwani akitokea mara mbili anaacha kuja kwako na kwenda kwingine, unakuwa umempoteza wateja."

Anawaasa wajasiriamali kuwa na bidhaa tofauti, si kwa kuwa na kitu ambacho hakijawahi kutokea au kuonekana sehemu hiyo, bali chenye upekee na ubora zaidi ya washindani.

Mariam anakiri kutambua wanawake wenzake kwenye baadhi ya maeneo nchini na hawapewi nafasi ya kumiliki ardhi, wakati dunia ya sasa mtu anapohitaji mkopo wa kujiendeleza katika biashara, ni lazima awe na cha kuweka rehani ambacho ni mali isiyohamishika kama ardhi.

UCHUMI

## SHAMBA LA NGERENGERE...

# Majibu yanayowahamisha wafugaji kutoka 'kusaka nyoka' hadi sayansi

## • Wafugaji wapishana na umaskini mlangoni

**Na Mwandishi Wetu**

LEO hii wakiulizwa wafugaji wanaoishi katika maeneo yanayozungukwa na Shamba la Mifugo la Serikali la Ngerengere mkoani Morogoro, jibu lao linaangukia katika 'kukombolewa kiuchumi' kutokana na kuchangia maendeleo yao katika ufugaji.

Wana kauli ya pamoja kwamba, kuwapo shamba hilo, kumewaondolea vikwazo mbalimbali, ikiwamo walivyokuwa wakihama maeneo yao.

Sasa wanabaki katika eneo lilelile, wakiwa wanawezesha kuendelea na ufugaji wakitumia mbinu za kisasa.



Baadhi ya mifugo inayopatikana kwenye Shamba la Serikali Ngerengere, mkoani Morogoro. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

**SAUTI YAO**

Kifuto Kimanga, mkazi na mfugaji wa Kiwege, anaeleza kwa muda mrefu alikuwa akifanya ufugaji wa kuhama na ulimsababisha yeye na familia yake kutokuwa na makazi maalum.

Kimanga anasema, kila siku walihangaika na kutumia muda mrefu poroni wakihangaikia kusaka na kupiga kambi katika maeneo ya kulishia mifugo na kuna wakati, waliingia kwenye migogoro na watumiaji wengine ardhi, baada ya mifugo yao kufanya uharibifu na hasa mashambani.

Anaeleza kutokana na uwapo wa shamba hilo lililoko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anasema sasa ameamua kuacha adha ya kuhama na kuamua kutafuta eneo la kudumu kwa ajili ya makazi na ufugaji wa kisasa, huku akiweka wazi mkombozi wake kifikra ni shamba la Ngerengere, lililompatia mbegu bora za mifugo wa kisasa.

"Uwapo wa shamba la LMU Ngerengere umewasaidia wafugaji kupata mbegu bora za mifugo kama ng'ombe, mbuzi na nguruwe kwa bei nzuri na mifugo hiyo inakuwa haraka, nyama nyingi na maziwa mengi," anasisitiza Kifuto.

Pia, anabainisha kwamba kuwapo shamba hilo, kunawaunganisha na msaada wa kitabibu kwa mifugo yao, kutoka kwa wataalamu wa mifugo waliopo katika shamba hilo, inayoambatana na utunzaji bora wa mifugo iliyopo.

Aidha, anadokeza mafanikio aliyopata kutokana na ufugaji bora na wa kisasa, kwani mwaka 2013 alijenga nyumba kubwa ya kisasa yenye uwezo wa kuhifadhi wakazi 24, inayokidhi haja zao na kupeleka watoto shule nzuri na za kisasa.

Kadhalika, anasema ameendelea kufaidika na mifugo hiyo kwa kuzalisha mbuzi kwa wingi na wanawauza kwa bei inayompa faida, tofauti na waliwanunua mbuzi kwenye shamba la LMU Ngerengere, huku akiorodhesha bei nafuu ya ununzi na mauzo ya mifugo kama mbuzi

Kifuto anajivunia kuwa na mbuzi wakubwa, wanaokua kwa haraka, wana nyama nyingi, makuzi yao yakipitia kauni muhimu za matunzo, ikiwamo chanjo, dawa za minyoo na lishe.

Esther Kilinga, mfugaji wa Kiwege, anaeleza kwamba amejipatia madume kutoka shambani hapo na kwa sasa ana ng'ombe 200, mradi uliofanikisha kujenga nyumba ya kisasa ya makazi na za wageni zinazowaingizia kipato na kuendesha maisha ya kila siku.

Kwa mujibu wa Kilinga, ni kiwango cha kipato kinchowawezesha hata kuchangia ujenzi wa nyumba ya ibada na kuwasomesha watoto kwa namna bora, katika shule anayoiita 'ya kisasa.'

Pia, mradi huo wa kuuza maziwa, unaendana na samli iliyo hai kwa wanakijiji Ngerengere na maeneo jirani, hatua inayowanufaisha na kuchangia pato la taifa.

Mfugaji mdogo na mkazi wa Ngerengere, Athumani Ramadhani, anajitambulisha alianza ufugaji mwaka 2018 akiwa na ng'ombe watatu, lakini sasa amefikisha 10.

Katika manufaa, hayuko mbali na wenzake na kuainisha faida alizozipata kujenga nyumba ya kisasa, kukidhi mahitaji ya familia yake ambayo hapo awali hali ya maisha ilikuwa mbaya.

Athumani anashukuru kuwapo shamba la LMU Ngerengere limewasaidia wafugaji kupata mbegu bora za mifugo inayowasaidia kuzalisha kwa wingi na kufundishwa kanuni za ufugaji bora na tiba kwa mifugo yao na kupata lita nane za maziwa kwa ng'ombe mmoja kwa siku.

Ana ombi kwaa serikali isaidie kuwajengea josho wafugaji majumbani, kwani namna ya kuhudumia mifugo huko sasa ni ngumu, kwa kuwa dawa haziwafikii vizuri na kuna wakati mifugo inakwepa dawa, hata juhudi za kufanikisha uogeshaji zinaangamia.

Kwa kutambua mchango wa Sekta ya Mifugo serikalini, iliamua kuwekeza katika mashamba ili kuyapa uwezo wa kuzalisha mifugo bora itakayosaidia kukuza kipato cha taifa na wananchi kwa ujumla.

Ngerengere, ni miongoni mwa mashamba matano ya serikali yaliyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

**MENEJA SHAMBA**

Meneja wa Shamba la Ngerengere, Saita Ole Kimosa, anasema lilianzishwa mwaka 1975 kama shamba la ng'ombe wa maziwa ambalo kabla lilifahamika kama 'Dairy Farm Company' lililokuwa chini ya watu binafsi na baadaye kufilisika, ndipo likabadilishwa jina na kuitwa LMU mwaka 2004 chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.


Anaeleza, lengo la kuanzishwa shamba hilo ni kuzalisha mifugo bora yenye tija na kuuziwa wananchi kwa bei ambayo ni rafiki na kujiingizia kipato na kusaidia wananchi kupata mbegu bora za mifugo.

Ole Kimosa anasema, hadi kufika Mei ya mwaka huu, 2020 lilikuwa maganyiko wa mifugo: ng'ombe 771, mbuzi 234 na nguruwe 201, uzalishaji ukiwa na tija.

Anataja aina ya mifugo iliyopo ni ng'ombe jamii za kisasa: Borani, Friesian na Chotara na kwa mbuzi, alitaja aina ya kutoa Afrika ya Kusini. Pia, nguruwe na mifugo mingine ya kisasa ipo.

Ole Kimosa, anataja mafanikio ya shamba, kwamba lina jumla ya mifugo takribani 1,206 na kuna mifugo mingi iliyozalishwa na kusambazwa, kwa kuwauzia wafugaji wadogo kwa bei ambayo ni rafiki katika Mkoa wa Morogoro na jirani Dar es Salaam.

Anafafanua kuwapo mifugo ya aina tatu, ambayo ni ng'ombe, mbuzi na nguruwe inayouzwa kwa wananchi kwa bei rafiki, ili kuwasaidia wananchi kupata mbegu bora za mifugo.



Meneja wa Shamba la Mifugo la Serikali Ngerengere, Saita Ole Kimosa.

**WAFUGAJI KUNUFAIKA**

Ole Kimosa anasema, hadi sasa wamewapatia wafugaji mitamba bora kwa bei nafuu, baadhi ya wameathiriwa ndani ya shamba la hilo la serikali, wanawauzia maziwa wananchi wanaozunguka shamba hilo na kuwapa maksai kwa ajili ya kulima.

Pia, anaeleza wafugaji wananufaika kwa mifugo yao kutibiwa na wanapata ushauri kutoka kwa wataalamu shambani, wakihamasishwa kutenga mifugo yao na kuibebesha mimba pamoja na kuuziwa madume bora, ili kuboresha ngombe wa asili na kuwauzia chotara.

Meneja huyo anafafanua kuwa, katika kipindi cha kiangazi, kuna lambo linalofahamika kama Mkobora ambalo limetengwa kwa ajili ya wananchi kunywesha mifugo yao, ili kusaidia ng'ombe na mifugo mingine isife kwa kukosa maji.

Anataja ugumu anaopata ni kuwapo miundombinu mibovu na iliyochakaapamoja uchakavu wa vitendea kazi, vyote vinafanya washindwe kutimiza baadhi ya majukumu yao ya kila siku na kutoka eneo moja kwenda lingine, kutokana na ubovu au kutokuwapo kabisa usafiri.

Meneja anaongeza, katika kipindi cha doria wananchi hukasirishwa na kuna wakati wanaamua kuchoma moto baadhi ya maeneo ya shamba.

Vivyo hivyo, inaendana na uvamizi mdogo wa wafugaji kuingiza mifugo na kulisha ndani ya mashamba ya watu na kisha wanatoka.


Kilichopo, anadokeza wanatarajia kila mwaka kufanya uzalishaji mkubwa wa mifugo, wauze na kupata fedha kwa ajili ya kurekebisha miundombinu ya shamba na kutatua changamoto zilizo ndani ya uwezo wao.



Nyumba ya Mfugaji, Kifuto Kimanga, ikiwa ni manufaa ya ufugaji wa kisasa katika Kijiji cha Kiwege – Ngerengere, mkoani Morogoro.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Mazingaombwe ya Giaboksi Mtambo wa Chuma!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

UCHAGUZI Mkuu wa mwaka huu na matokeo yake, umerudisha fikra zangu nyuma, mpaka nilipokuwa shule ya msingi miaka ya sabini.

Kichwani nimesikia upya kengele ya kumaliza vipindi saa 10 jioni, ambayo kila ikilia ilishangiliwa na kila mwanafunzi. Kwamba tunakwenda mstarini kujipanga kupokea matangazo ya mwalimu wa zamu na maagizo ya kesho na kusepa.

Nimekumbuka siku tulipojipanga na kisha kuletewa mgeni kutoka chumba cha walimu, mgeni Mhindi aliyevalia shati jeupe, tai nyeusi, kaptula nyeupe, soksi nyeupe na viatu vyeusi.

Mwalimu wa zamu akatutambulisha kuwa anaitwa Profeseri. Naye akatusalimia kwa Kiswahili na kujitambulisha, kuwa ni mtaalamu wa mazingaombwe na katika kututhibitishia, akatoa karata na kuziunganisha kimaajabu, kuwa kama kamba.

Tulipomshangilia huku akitumia kauli ya 'Giaboksi Mtambo wa Chuma', akaahidi kuwa kesho atakuja kutuonesha maajabu zaidi, ikiwa ni pamoja na kupasua mtu bila ganzi na kumtoa alivyokula. Tulishika vichwa na kuziba midomo.

Katika mshangao huo, akatutaka kila mtu kesho aje na thumni (Sh. 50) kama kiingilio. Kisha tukatawanyika kila mtu na wazo la jinsi ya kumwingia mzazi aitoe hiyo thumni.

Kesho yake Profeseri akaja saa nane, tuliokuwa na thumni tukaingia darasa moja tayari kuoneshwa hayo maajabu. Akaonesha maajabu yake ikiwa ni pamoja na kutafuna karatasi na kutapika noti nyingi. Kutafuna wembe na kutoa sindano nyiingi, nakadhalika.

Ukafika wakati wa kupasua mtu, akitakiwa wa kujitolea. Nilijishangaa nimejitolea mimi kupasuliwa, bila kuogopa matokeo yake.Sijui ujasiri ule niliuazima kwa nani siku hiyo!

Nikakalishwa juu ya meza na kulishwa ndizi kubwa tatu harakaharaka, na kulazwa chali na kufunikwa gubigubi. Nikasikia nikibonyezwa-bonyezwa tumbo huku nikisikia wanafunzi wenzangu wakikatazwa kupiga kelele.

"Mkipiga kelele tu huyu hataamka tena atakuwa amekufa, kaeni kimya, mkiangalia jinsi nitakavyompasua na kumtoa ndizi alizokula," alionya Profeseri. Na kweli kwa hofu, chumba kizima kilizizima.

Baada ya hapo nikafungwa pamba na bandeji tumboni na kuamshwa. Nikasikia wenzangu wanashangilia. Nikaogopa hata kugusa tumbo nisije nikafumua 'mshono'. Profeseri akaniruhusu kuondoka, huku wenzangu wakinipokea kwa mshangao na kutoamini.

Baadaye Profeseri akanichukua chemba na kunipa kiasi cha fedha kama shukurani yake, kwamba sikumwangusha na akanifundisha mchezo mmoja ambao hata leo hii ukiniuliza, sikumbuki alinifundisha mchezo gani. Mazingaombwe bwana acha tu!

Uchaguzi huu umenishitua kuona vigogo wakisambaratishwa. Mpaka sasa bado siamini, inawezekana hata wenzangu hawaamini hilo. Walioshinda wameshinda sawa, lakini kwa tofauti hizi za kura mh! Hapo ndipo ninapopasuliwa tumbo kwenye mazingaombwe.

Hebu tufuataneni hapa, muone ninavyozinguliwa na mazingaombwe haya: Mdee kupata kura 33,000 huku Askofu Gwajima akipata 194,000! Mchungaji Msigwa akipata 29,000 dhidi ya 36,000 za Jesca! Eti Sugu akisugua 38,000, Tulia akitulia na 75,000!

Haya, Waitara katoka Ukonga kaenda kumkuta mwenyeji Heche na kuzoa 36,000 dhidi ya 19,000! Haitoshi, Matiko anaambulia 11,000 dhidi ya 18,000 za Kembaki! Wajina wake, binti Bulaya anaambulia 13,000 akibwagwa na Maboto mwenye 31,000!

Mara Zitto eti anaangukia pua kwa Ng'enda anayepata 28,000 yeye akiambulia 21,000! Nyalandu naye anaambulia 16,000 akibwagwa na Ighondo anayepata kura 44,000.

Duh huko Hai, kigogo kabisa Mbowe eti anaambulia 28,000 akitumbuliwa na Mafuwe anayejizolea 90,000, Selasini akiadhirika na kura 416 dhidi ya 48,000 za Mkenda, huku Lema akiburuzwa na Gambo mwenye 82,000 dhidi ya 46,000.

Silinde aliyehama kutoka Chadema na Momba alikokuwa 2015 anakuja Tunduma na kumviringaviringa Mwakajoka, akipata 44,000 dhidi ya 12,000. Mimi kwangu bado naona kama mazingaombwe. Yawezekana ni kweli na tuamini ili maisha yaendelee. Alamsiki!

BIASHARA

Na Julieth Mkireri, KIBITI

# RC Pwani: Mwaka huu tumepania mazito kwenye uzalishaji korosho

## • Azindua na kufuatilia sentensi zake



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, akiwa katika ghala la kuhifadhi Korosho Mkuranga kukagua namna zinavyohifadhiwa kabla ya kuuzwa.

KOROSHO ni moja ya mazao ya biashara yanayotegemewa kukuza uchumi katika Mkoa wa Pwani ikifuatiwa na ufuta na inaelezwa, wastani wa asilimia 80 hadi 90 ya wakazi Mkoa wa Pwani, ama wanalima au kujishughulisha nalo.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, mbali ya kujikita kuhamasisha ujenzi wa viwanda na kuufanya mkoa huo kuongoza ajenda hiyo, sasa ameamua kuvalia njuga korosho.

Ndikilo amekuwa na vikao na wadau wa korosho na amevitumia kusisitiza usafi mashambani, pia uhifadhi mzuri ili soko la korosho kimkoa, uwe na thamani kubwa ndani na nje ya nchi.

Anasema sio kazi rahisi kushuhudia korosho za mikoa mingine katika minada yake zikiuzwa kwa bei ya juu, huku Pwani ikikosa soko, jambo analoahidi hatokubaliana nalo hata kidogo.

"Ninachokitaka ni wakulima kufuata taratibu na kanuni za uhifadhi wa korosho, ili zinapofika kwenye maghala wanunuzi wavutiwe nazo nisingependa kusikia tumekosa soko kutokana na ubora wa korosho zetu, hili kwa Pwani tunalipinga na nitapambana lisitokee," anaahidi .

Mkuu wa Mkoa, kila mara amekuwa akiagiza katika vikao vyake na wadau wa korosho na kukutana na maofisa ugani wa halmashauri za mkoa, anawatembelea wakulima na kuwaongezea elimu ya kilimo cha zao hilo, hata namna ya kuzihifadhi zinapotoka shamba.

Anasema ili kupata Korosho bora maandalizi yake yanatakiwa kufanyika tangu zikiwa shambani na mkulima kuwa makini kwa kila hatua kwa kufanya hivyo, zitapatikana zenye daraja la juu zitakazouzika kwa urahisi.

"Ninasisitiza utunzaji mzuri wa korosho kuwa na sehemu safi na salama za kuhifadhia kabla ya kuziweka kwenye magunia hii itasaidia kuwa na Korosho bora," anatamka.

**STAKABADHI GHALANI**

Akielezea kuhusiana na mfumo wa stakabadhi ghalani ulivyoleta faida katika misimu miwili iliyopita, Mhandisi

Ndikilo anasema: "Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ulianza katika mkoa rasmi mwaka 2017/2018, ambayo tani 20,650.03 zilikusanywa na kuingiza zaidi ya Sh. bilioni 59"

Ndikilo anasema, katika msimu wa mwaka 2018/2019 uzalishaji uliongezeka kufikia tani 23,266.7 zilizokusanywa na kuingiza shilingi billion 63.

Anasema, mafanikio hayo yalitokana na njia bora katika maandalizi na hifadhi ya korosho sokoni na katika

Msimu uliopita, anataja uzalishaji uliyumba kutokana na hali mbaya hewa, upepo na mvua nyingi zilizonyesha, hata kuufanya mkoa kuishia kukusaya jumla ya tani 16,317.170 na kuingiza Sh. bilioni 9.9.

**MSIMU ULIOZINDILIWA**

Katika uzinduzi wa mnada msimu uliopo, korosho daraja la kwanza liliuzwa kwa Sh. 2153 huku daraja la pili likisubiri mnada mwingine kutokana na wakulima kutoridhia bei ya Sh.1400.

Akizungumza na wakulima viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) Mhandisi Ndikilo, anaeleza kuwapo mambo yanayotakiwa kutekelezwa na wahusika, pasipo visingizio, mahsusi akitaja usimamizi wa ukusanyaji mzuri wa korosho.

Mhandisi Ndikilo anawataka viongozi wa ngazi zote kulisimamia hilo na kuhakikisha korosho zinaelekezwa kwenye mfumo wa Stakabadhi Ghalani, pasipo kutoa nafasi kwa njia zisizo rasmi.

Katika mnada huo uliozinduliwa Novemba 11, huko Kibiti, anawaonya viongozi wa AMCOS na hasa makatibu wake, kuwa makini na kujiepusha na ubadhilifu wa korosho za wakulima.

"Upotevu wa korosho za wakulima kwa kisingizio cha 'unyaufu' haukubaliki na wahusika wote watawajibishwa. Kinachotakiwa ni wakulima wanaoleta korosho jina na kilo zao ziwekwe wazi," anaeleza Ndikilo.

Mkuu huyo wa mkoa, pia anatumia nafasi hiyo kuwaasa wakulima kuendeleza ubora wa korosho na kujiepusha na kuchanganya vitu vingine.

Anatoa agizo pia kwa wakuu wa wilaya kuhimiza Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), kuhakikisha hali ya barabara zinazotoka shambani hadi kwenye maghala ziko vizuri, kurahisisha usafirishaji wa korosho.

Ndikilo pia, anahimiza Chama Kikuu cha Ushirika (CORECU) na AMCOS, kuhakikisha wakulima wanalipwa kwa wakati baada ya korosho zao kuuzwa.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Shangwe Twamala, anasema hadi kufikia Novemba 10 (iliyopita) vyama vya msingi vimekusanya jumla ya kilo 3,709,167 kutoka Mkuranga ni kilo 909,375; Kibiti 1,519,700; Rufiji 1,174,592; Mafia kilo 3,200; Kisarawe 52,300; na Kibaha 50,000.

**KATIBU TAWALA MSAIDIZI**

Anasema hadi kufikia Novemba 11 maghala makuu yanayofanya kazi ni Ikwiriri Wilaya ya Rufiji, Kibiti na Mwanambaya Mkuranga.

Twamala anabainisha kuwa mnada huo ulihusisha uuzaji wa kilo 2,073,293 sawa na asilimia 55.9 ya korosho zote zilizokusanywa na AMCOS na kilo 1,740,054, zipo kwenye maghala makuu ya Ikwiriri (kilo 770,677, Kibiti 482,132 na Mkuranga kilo 487,245.

Aidha, kilo 333,239 zinaelezwa zipo katika ghala la kampuni ya Biotan Mkuranga, akifafanua kuhusiana na madaraja ya korosho, akieleza kwamba, kati ya kilo 2,073,293 zilizolengwa kuuzwa, kuna 512,786 za daraja, ikiwa ni asilimia 24.7 na 1,560,507 na daraja la pili sawa na asilimia 75.3.

**WAKULIMA**

Rashid Mohamed, ni mkulima wa Njopeka Rufiji, rai yake kwake anamuomba mkuu wa mkoa kusimamia pembejeo zifike kwa wakati lakini pia changamoto zinazosababisha kushuka kwa madaraja ya zao hilo.

Naye, Abdul Idd, mkazi wa Rufiji, aliwashauri wakulima kuridhia bei iliyotajwa na wanunuzi na zilizobaki ziuzwe katika mnada wa pili.

Katika mnada huo wa korosho msimu uliopita, mauzo ya korosho Mkoa wa Pwani, kilo zilizoingia sokoni kwa daraja la kwanza ni 260,558; daraja la pili ni kilo 1,479,496 kwa bei ya juu Sh.2, 153 ya chini Sh. 2,052.

Aidha, korosho daraja la kwanza ziliuzwa zote huku la pili likisubiri mnada wa awamu ya pili kutokana na wakulima kutoridhishwa na bei iliyotajwa na wanunuzi.



Mhandisi Evarist Ndikilo, akiangalia namna korosho zinavyokatwa kutenganisha nzima na zisizofaa katika ghala la Mkuranga. **PICHA ZOTE: JULIETH MKIRERI.**

# Ndugai mgeni maadhimisho wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, anatarajia kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani yatakayofanyika Kongwa mkoani hapa ambayo yatashirikisha watu 500.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wantalima, akizungumza na waandishi wa habari, alisema maadhimisho hayo yatafanyika Desemba Mosi hadi 3, mwaka huu.

Ngw'antalima alisema Spika wa Bunge atatumia nafasi hiyo kukabidhi vifaa visaidizi kwa watu wenye ulemavu wa wilaya hiyo.

Katibu huyo alisema pamoja na kukabidhi vifaa, pia kutakuwa na utoaji wa elimu itakayotolewa na wadau wenza wa shirikisho hilo.

Alisema miongoni mwa elimu hiyo kuielimisha jamii kuondokana na mila potofu iliyojengeka miongoni mwa watu kuacha tabia ya kuwabagua na kuwatenga watu wenye ulemavu.

"Elimu hiyo ni mategemeo yetu kuona watu wenye ulemavu wakipatiwa haki zao za kimsingi ikiwamo afya, elimu na haki sawa kama ilivyo kwa wengine ambao hawana ulemavu wowote," alisema.

**Elimu hiyo ni mategemeo yetu kuona watu wenye ulemavu wakipatiwa haki zao za kimsingi ikiwamo afya, elimu na haki sawa kama ilivyo kwa wengine ambao hawana ulemavu wowote.**

# Tatizo la mfumo majitaka bado kubwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA inakabiliwa na tatizo la mifumo ya majitaka huku iliyopo ikiwa haikidhi mahitaji ya watu hasa katika maeneo ya mijini, imeelezwa.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeombwa kuwekeza fedha nyingi zaidi katika mipango miji pamoja na mifumo ya majitaka.

Akizungumzia jana na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Choo Duniani, Ofisa Mawasiliano na Kampeni wa Shirika la WaterAid Tanzania, Neema Kimaro, alisema mwaka 2016 miji 10 tu nchini ilikuwa na mifumo ya majitaka ambayo bado haikukidhi mahitaji ya watu.

"Hivi sasa miundombinu ya choo inaelemewa kutokana na ongezeko la ukuaji wa miji na majiji nchini Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa kulingana na utafiti uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2017 na ripoti ya kitaifa ya mazingira, hadi kufikia mwaka 2017, inakadiriwa kuwa asilimia 70 hadi 80 ya Watanzania waishio mjini hawakuwa na miundombinu imara ya vyoo na huduma za uzoaji wa taka hasa za chooni.

"Katika miaka ya hivi karibuni, sote tumekuwa mashahidi wa namna mvua kubwa zimesababisha maafa makubwa kwenye biashara za watu mbalimbali, makazi pamoja na miundombinu ya vyoo, na kuacha watu bila makazi na sehemu ya kujisaidia," alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na hali hiyo mwaka mwaka 2016, shirika hilo liliwapatia watu wanaojihusisha na biashara ya kuzoa au kuchukua maji taka, mikopo yenye riba nafuu ili kukuza biashara yao.

"Mikopo hii huitumia kununulia vifaa vya kazi kama vile buti na koleo na kusaidia wao wenyewe wajikinge na magonjwa katika kazi zao, hivyo kufikia watu wengi zaidi na kupunguza adha ya kujaa chemba za vyoo katika miji yenye msongamano wa watu," alisema.

Hata hivyo, aliomba serikali na wadau wa usafi wa mazingira nchini, kuwekeza fedha nyingi zaidi katika mipango miji pamoja na mifumo ya majitaka, ili kila mahali kuwe na choo bora na hali ya usafi katika mifumo ya choo sehemu anayoishi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha maafa makubwa kwenye miundombinu na hivyo kupunguza magonjwa yanayosababishwa na kula kinyesi.

"Serikali na wadau ikiwa ni pamoja na sisi WaterAid Tanzania, tukae pamoja na kujadili ni kwa namna gani tunaweza kuboresha miundombinu hasa katika maeneo ya mijini ili kuhakikisha kuwa tunasaidia jamii zetu kuwa na vyoo ambavyo vitahimili mabadiliko ya tabia nchi na vyoo vya umma vijali mahitaji ya watu wenye ulemavu," alisema.

Aidha, alisema majadiliano hayo na bajeti vifikiriwe ili kuongeza huduma katika vijiji na miji.

**Hatua hiyo itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha maafa makubwa kwenye miundombinu na hivyo kupunguza magonjwa yanayosababishwa na kula kinyesi.**




Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Emanuel Kayuni (katikati), akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa baraza dogo la wafanyakazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoji, jijini Dodoma jana. Kulia ni Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, John Masunga na Katibu wa baraza hilo, Maria Lema. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RAS asema usimamizi wa mirathi bado kitendawili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kessy Maduka, amesema licha ya uwapo wa sheria mahususi zilizotungwa kwa ajili ya kuwezesha usimamizi bora wa mirathi, bado kuna usimamizi mbovu wa mirathi kwenye jamii.

Maduka aliyasema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria, jijini hapa.

Alisema kwa muda mrefu serikali imekuwa ikitambua uwepo wa tatizo la wananchi wengi kutokuwa na uelewa wa kisheria katika masuala ya usimamizi wa mirathi katika ngazi ya familia hali inayochangia watu wengi kudhulumiwa haki zao za msingi.

Kwa mujibu wa Maduka, moja ya athari za kutokuwa na usimamizi bora wa mirathi ni familia kuingia katika migogoro, kugawana mali, kupoteza mali na kufilisika.

"Kwa kutambua uzito wa tatizo hilo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikifanya juhudi za kuhakikisha juhudi za msaada wa kisheria kuhusiana na masuala ya usimamizi wa mirathi unawafikia wananchi wengi kadiri inavyowezekana," alisema.

Pia alisema serikali imefanya juhudi za kuanzisha sheria mahususi ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria pamoja na kanuni zake za mwaka 2018.

Alisema sheria hiyo inaweka msingi wa utaratibu mzima wa kuratibu utoaji huduma za kisheria, inaanzisha Bodi ya Taifa ya Msaada wa Kisheria inaweka ulazima wa kusajili watoa msaada wa kisheria kwa kuweka vigezo na sifa za mtu au taasisi inayoweza kusajiliwa kutoa huduma za sheria.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Katiba na Ufuatiliaji Haki Wizara ya Katiba na Sheria, Burton Anosisye, alisema wizara itaendelea kutumia fursa zilizopo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuyajengea uwezo mabaraza ya kata ambayo kimsingi ndiyo ngazi ya awali ya usuluhishi katika jamii.

Alisema kuwa wizara inafahamu kuwa watoa misaada wa kisheria wamejikita katika kuelimisha jamii, na misingi ya usimamizi bora wa mirathi, ili kuondoa kero na dhuluma kwa wananchi.

"Tuna imani katika siku hii wananchi na jamii kwa ujumla wataelewa kwa undani masuala ya kisheria na kuondokana na dhuluma inayotokana na usimamizi mbaya wa mirathi na kusababisha wanufaika kukosa haki zao na hivyo kubaki maskini tofauti na malezi waliyokuwa wanayapata wakati wa uhai wa wazazi wao," alisema.





# Walalamikia Hospitali Rungwe kukosa X-Ray

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya inadaiwa kukosa kipimo cha mionzi (X-Ray) kwa zaidi ya miezi saba hali inayowalazimu wagonjwa wanaohitaji kipimo hicho, kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo jijini Mbeya.

Mmoja wa wananchi hao waliolalamikia kukosa huduma hiyo ni Bryson Mwakitalima, mkazi wa Jiji la Mbeya aliyekuwa anauguza vijana wake watatu waliopata ajali ya pikipiki wilayani Rungwe.

Alisema baada ya vijana hao kupata ajali walikimbizwa katika hospitali hiyo ijulikanayo kwa jina la Mkandana, lakini walipofika hospitalini hapo waliambiwa kipimo hicho hakipo, na ndipo akalazimika kumhamisha mmoja wa majeruhi hao aliyekuwa na hali mbaya.

"Nilipofika hospitalini pale nilishangaa kuambiwa eti Hospitali ya Wilaya haina kipimo cha X-Ray, lakini kwa sababu mmoja wa wajomba zangu hao alikuwa na hali mbaya nililazimika kumpeleka katika Hospitali ya Mission ya Igogwe zaidi ya kilimita 10," alisema Mwakitalima.

**Kwa sasa mashine mpya zimenunuliwa na serikali kwa gharama ya Sh. milioni 330 na zinatarajiwa kufika wakati wowote, huku akibainisha kuwa jengo kwa ajili ya vipimo hivyo limeshakamilika.**

Alisema ni aibu Hospitali ya Wilaya kukosa kipimo kama hicho hasa kipindi hiki ambacho nchi imeingia kwenye uchumi wa kati, na akaiomba serikali kushughulikia tatizo hilo haraka ili wananchi wasihangaike.

Naye mmoja wa majeruhi wa ajali waliofika katika hospitali hiyo, Vumilia Hosea, aliyelazwa hospitali hiyo ya Makandana, alisema mbali na hospitali hiyo kukosa huduma hiyo pia kuna tatizo la uwepo wa huduma mbovu.

Alisema alitibiwa kwa muda na akaruhusiwa kuondoka huku akiwa na maumivu makali, hali iliyowafanya ndugu zake badala ya kwenda naye nyumbani wakaamua kumpeleka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Alisema baada ya kufika katika hospitali hiyo, alilazwa kwa siku nne akitibiwa majeraha ambayo katika Hospitali ya Makandana aliambiwa amepona.

"Wakati natoka hospitalini pale nilikuwa na hali mbaya, lakini wao waliniambia nimepona, hivyo wakanitaka nirudi nyumbani, ndugu zangu walipokuta nalalamika na kupepesuka njiani wakaamua kubadili maamuzi na kunipeleka Mbeya," alisema Vumilia.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. John Mrina, alithibitisha kutokuwapo kwa huduma hiyo, huku akisema zipo mashine za zamani ambazo hazifanyi kazi.

Alisema kwa sasa mashine mpya zimenunuliwa na serikali kwa gharama ya Sh. milioni 330 na zinatarajiwa kufika wakati wowote, huku akibainisha kuwa jengo kwa ajili ya vipimo hivyo limeshakamilika.

"Jengo limekamilika, lakini tunawasubiri wataalamu wa mionzi kutoka Tume ya Nguvu za Atomic (TAEC) iliyopo mkoani Arusha ambao wanatarajiwa kufika muda wowote kwa ajili ya kupima jengo letu kama linafaa kutumika," alisema Dk. Mrina.



Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, akiwasilisha taarifa ya kilimo, wakati wa mkutano wa kutathmini rasimu ya kilimo ya mkoa huo ya mwaka wa kilimo 2020/2021, mkoani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mabadiliko tabianchi kuathiri wanawake

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TATIZO la kijiografia na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na uharibifu wa mazingira imekuwa kikwazo cha kuwainua wanawake kiuchumi kutokana na kuathiri shughuli zao za uzalishaji hususani kilimo.

Hayo yalisemwa jana na Mjumbe wa Bodi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jovita Mlay, wakati wa uzinduzi wa tamasha la siku tatu la jinsia kwa ngazi ya wilaya ambalo limefanyika katika kijiji cha Hatwelo Kata ya Ijombe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Mlay alisema kuwa mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali hususani vijijini yamesababisha mvua kusuasua au kukosekana kabisa na kuathiri shughuli za kilimo zinazofanywa na wanawake, hivyo kushindwa kufikia malengo yao.

Kwa mujibu wa Mlay, mvua inaponyesha kidogo au inapokosekana kabisa inasababisha wanawake ambao wanajihisisha na kilimo kupata mazao machache, na kusababisha kushindwa kuinuka kiuchumi, huku akisisitiza umuhimu wa jamii kulinda na kuhifadhi mazingira.

"Lakini katika baadhi ya kata zimekumbwa na ukosefu au upatikanaji duni wa maji, jamii zimekosa vyanzo vya uhakika vya maji na waathirika wakubwa ni wanawake, hili eneo pia liangaliwe kwa upekee," alisema.

Katika hatua nyingine alisema pamoja na mafanikio ya kupinga ukatili wa kijinsia, lakini bado kuna mfumo dume ambao umekuwa ukirudisha nyuma juhudi za serikali katika kutekeleza mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alisema dhana ya usawa kijinsia ni suala la maendeleo na sio vinginevyo.

Alisema lengo ni kujenga nguvu ya pamoja na kuhakikisha rasilimali za nchi zinagawanywa katika haki na usawa wa familia, jamii, serikali za mitaa na serikali kuu zinagawanya bajeti zenye mlengo wa kijinsia.

"Kama wanawake ni zaidi ya asilimia 50, vijana ni zaidi ya asilimia 60 sidhani kama kuna mpango wowote wa maendeleo ukiwaacha nyuma utakwenda vizuri, ukiyaacha nyuma hayo makundi maendeleo yatasuasua sana hayatakwenda vizuri," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema serikali haitawavumilia watu wote ambao watabainika kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia pamoja na watoto ikiwamo ubakaji na kuwapa ujauzito wanafunzi.

# Mkoa kuongeza uzalishaji wa mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema inakusudia kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara, ili kuimarisha uchumi wa mkoa na kuwa na uhakika wa chakula kwa wananchi.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa huo, Said Madito, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha kujadili rasimu ya Mpango Mkakati wa kilimo wa miaka mitano kuanzia mwaka 2020/2025 ambao uliwahusisha wadau mbalimbali wa kilimo.

Madito alisema katika mpango huo wa serikali, wanakusudia kuongeza uzalishaji wa mazao matano ya kipaumbele ya chakula ambayo ni mahindi, mpunga, maharage, viazi mviringo na ndizi ambayo yanalimwa katika maeneo tofauti ya mkoa.

Aidha, Madito alisema mkoa huo pia unakusudia kuongeza uzalishaji wa mazao saba ya kimkakati ya kibiashara ambayo ni kahawa, chai, tumbaku, korosho, kaka, pareto na michikichi.

"Katika kipindi cha miaka mitano, Mkoa utaendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinakuwa ni chenye tija na kinachotumia teknolojia za kisasa ili kufikia azma ya kuwa na utoshelevu wa chakula na kuinua uchumi," alisema Madito.

Alisema baadhi ya mipango ya kuongeza uzalishaji huo ni pamoja na kuboresha kilimo cha umwagiliaji, kuongeza usambazaji na matumizi ya pembejeo za kilimo kwa gharama nafuu na kuhamasisha uzalishaji wa miche bora ya mazao ya kimkakati.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za serikali ni kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2015/2020 Mkoa wa Mbeya ulikuwa unajitosheleza kwa chakula.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhakikisha wanafuatilia ufanisi wa uzalishaji wa mazao hayo kwenye maeneo yao.

Alisema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa na hivyo akasisitiza rasimu iliyoandaliwa iboreshwe kwa kuyaingiza mapendekezo ya wadau ili tija inayokusudiwa ipatikane ndani ya kipindi kilichokusudiwa.

Alisema asilimia kubwa ya mambo yaliyomo kwenye mpango huo yanatokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) hivyo isipotekelezwa vizuri viongozi hao watatakiwa kulaumiwa.



# TAMWA yashauri wajasiriamali kuongeza ufanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar kimewataka wajasiriamali kuhakikisha wanaongeza ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa, ili kuwa kivutio kwa lengo la kuongeza kipato kwa manufaa yao.

Akizungumza jana na wajasiriamali hao, Ofisa Uwezeshaji Uchumi, Nairat Abdalla Ali, aliwataka wajasiriamali hao kutumia fursa wanazopatiwa kila siku zikiwamo za kujengewa uwezo kuwa sehemu ya mabadiliko.

Alisema kawaida ili mteja anunue bidhaa anahitaji kuona ubora wake zisizokua na kiwango haziwezi kufanya vizuri sokoni.

Naye Ofisa Masoko wa TAMWA, Zanzibar, Muhidini Ramadhan, aliwataka wajasiriamali hao kutokata tamaa na changamoto zinazowakabili.

Alisema licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali wakati wa uzalishaji wa bidhaa hizo, hawapaswi kuzichukua changamoto hizo kuwa sababu ya kukata tamaa na kuacha kuzalisha.

"Sisi TAMWA tunafahamu mna changamoto nyingi zinazowakabili, lakini nawaomba msikate tamaa na zigeuzeni changamoto hizo kuwa sehemu ya fursa," alisema.

Kadhalika, alisema miongoni mwa njia kuu zitazowasaidia wajasiriamali hao kupiga hatua zaidi ni kujenga ushirikiano baina yao na wadau wengine mbalimbali ambao wanaamini watakawa miongoni mwa nyenzo za kukuza fursa zaidi ikiwamo kupata masoko.

Baadhi ya wajasiriamali hao walisema miongoni mwa changamoto wanazokutana nazo ni upatikanaji wa vifungashio vya bidhaa zao wanapomaliza kuzalisha.

Miongoni mwao, Faida Mohamed Shaibu, alisema ni pamoja na uhaba wa masoko ya uuzaji wa bidhaa hizo na vifungashio vimekuwa tatizo kubwa kwao.

"Kutokana na mazingira ya aina hii wakati mwingine tunalazimika kubaki na bidhaa zetu majumbani bila ya kuwa na sehemu sahihi ya kuhifadhi na kusababisha kuharibika," alisema.

# Dk. Mwinyi aanza kutumbua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewatumbua Mkurugenzi Mkuu wa Afya, Wizara ya Afya, Dk. Jamala Adam Talib na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Dk. Ali Salum Ali.

Dk. Mwinyi amefuta nafasi za wakurugenzi hao juzi, baada ya kufanya ziara ya ghafla katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kusikiliza kero za wananchi na wagonjwa na kutoridhishwa na utoaji wa huduma hospitalini hapo.

Pia, Dk. Hussein juzi alikutana na wafanyabiashara katika eneo la Kijangwani na kabla ya ziara yake hiyo Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Hassan Khatib, alitoa tamko la kutaka wafanyabiashara wa eneo hilo kuondoka.

**Hivi sasa wateja wao wamelishalizoea soko hilo la Kijangwani wanatakiwa kuondoka na kupelekwa eneo jingine jipya, jambo ambalo linawapa hofu kubwa kupoteza mitaji yao.**

Wakati alipokutana na wafanyabiashara hao walimweleza Rais Mwinyi, kitendo cha kuhama kutoka eneo moja kwenda jingine kunasababishia kufa kwa mitaji yao ya biashara.

"Hatukatai kuhama katika soko hili ila tunaomba tutafutiwe sehemu iliyokuwa nzuri maana kuhama hama huku kunatuathiri sana," alisema Juma Haji kwa niaba ya wafanyabiashara wenzake.

Alisema kipindi cha corona waliondolewa katika Soko la Darajani na kupelekwa eneo la Kijangwani na wafanyabiashara wengi walipoteza mitaji yao na kushindwa kuendelea na biashara.

Alisema hivi sasa wateja wao wamelishalizoea soko hilo la Kijangwani wanatakiwa kuondoka na kupelekwa eneo jingine jipya, jambo ambalo linawapa hofu kubwa kupoteza mitaji yao.

Alisema eneo walilopangiwa kufanya biashara si rafiki kwa madai kuwa watakosa wateja kwa kuwa halijazoeleka.

Alisema kuhamishwa katika soko hilo na kupelekwa eneo la Jitimai hawajaliafiki na kumwomba Rais kuwasaidia ili kuwa na sehemu ya kudumu.

Naye Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, aliutaka uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Mjini, Baraza la Manispaa na wafanyabiashara wa Kijangwani kukaa pamoja na kutafuta sehemu ya kudumu itakayokuwa nzuri kwa wafanyabiashara ili kufanya biashara zao kwa urahisi.

Alisema kukaa pamoja kutasaidia kutafuta sehemu iliyokuwa nzuri ikiwamo miundombinu bora ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kufanyabiashara vizuri.

Alisema wote wanafahamu soko hilo si la kudumu na lipo kwa muda na kuwataka kipindi hiki cha kutafuta eneo jingine wabaki hapo hadi sehemu itakapopatikana.

Dk. Mwinyi alisema, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imesema kuwa itatekeleza mazingira bora ya wafanyabiashara na kuwapa vitambulisho ili kodi zisitolewe kila siku na kwamba ahadi aliyoitoa ipo kwa kuona mazingira yanakuwa mazuri ya kufanyabiashara.

"Nakuahidini nitakuwa wa kwanza kulisimamia suala hili kwa kuwa nimeahidi na nimekuja hapa nitakuwa wa kwanza kulisimamia hili," alisema huku akishangiliwa na wafanyabiashara hao.

Akizungumzia mradi wa kituo cha gari za abiria katika eneo hilo la Kijangwani, alisema mradi huo unalengo la kuwawekea mazingira mazuri ya biashara, hivyo wafanyabiashara hao hawana budi kukubaliana nao ili kuwapo kwa mazingira mazuri.

"Nauagiza uongozi wa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kuharakisha kutafuta eneo ambalo litakuwa la kudumu wafanyabiashara kama hamuwezi kulipata mimi nitalipata," alisema.

Alisema kuwa mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa na mji safi kila sehemu na kuwataka wafanyabiashara hao kuendeleza usafi wa mji.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib, alisema kuwa uamuzi wa kuondolewa wafanyabiashara hao upo katika mpango wa serikali ambao sehemu hiyo inataka kujengwa soko kubwa pamoja sehemu ya kituo cha daladala cha kisasa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipata maelezo kutoka kwa Dk. Slim Mgeni, alipotembelea kitengo cha macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wanafunzi wanaosoma nje ya nchi wapewa somo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrissa Muslim Hija, amewataka wanafunzi wanaopata nafasi za masomo nje ya nchi kuhakikisha wanasoma kwa bidii ili kufikia malengo.

Alisema hayo jana wakati wa hafla fupi ya kuwaaga wanafunzi waliopata ufadhili wa masomo nje ya nchi, chini ya Taasisi ya Carry Vision, Mazizini mjini Unguja.

Alisema kusoma mbali na mazingira ya nyumbani kunahitaji ustahimilivu wa hali ya juu na mwenye kustahamili ndiye mwenye mafanikio mazuri ya hapo baadaye.

Aliwasisitiza kuendelea kulinda mila, silka na utamaduni wa nchi yao kwa kuwa wazalendo na kurejea nyumbani wanapomaliza masomo ili kuendeleza uchumi wa nchi yao.

Dk. Idrisa aliwasihi wanafunzi hao kushirikiana baina yao hasa katika masomo ili kufikia mafanikio ya kufaulu vizuri na kuieletea sifa nchi yao.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo na Uratibu wa Elimu ya Juu, Aida Moulid Juma, alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ndiyo inayosimamia elimu nchini kwa ngazi zote na kuwataka wanafunzi wanaoenda masomoni kuhakikisha wanaporudi masomoni kutoa taarifa wizarani kama walivyotoa wakati wa kuondoka ili kusaidia taifa kujua wahitimu wake katika fani mbalimbali na kuwaajiri.

Naye Mkurugenzi wa taasisi inayoshughulikia masuala ya udahili na udhamini wa elimu ya juu kwa vyuo vya nje, Carry Vision, Yussuf Suleiman, alisema kuna wanafunzi wamefadhiliwa ada za chuo na huduma zote na wengine wamefadhiliwa ada pekee na kupata mkopo kwa ajili ya huduma nyingine.

Wanafunzi hao wameipongeza Wizara ya Elimu kwa nasaha zao ambazo zitawasaidia kipindi chote cha masomo, jumla ya wanafunzi 27, wamepata udhamini wa masomo wakiwamo wanawake 21 na wanaume sita, katika fani mbalimbali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

*NIPASHE NI JIBU LAKO*
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**RUTH ERASTO NYONDO** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.1340/0524** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **LWANGA** mwaka **2020**,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa:**
**DAR/KIG/RB/809614/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



1160073O2

**GIDEON MBETA RWEGERERA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0849-0080** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia Musoma Day Sekondary mwaka 2000. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0176-0501** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia Lusangi Moravian Junior Seminary mwaka 2003. Leaving Certificate ya kidato cha nne iliyotolewa na Musoma Day Secondary mwaka 2000. Leaving Certificate ya kidato cha sita iliyotolewa na Lusangi Moravian Junior Seminary mwaka 2003. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/739822/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



116006102

**BIULEDI A. MAISHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha DIPLOMA IN SECONDARY EDUCATION chenye namba **E0505-0006** kilichotolewa na **KOROGWE TEACHER'S COLLEGE** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**
**PWA/BAG/RB/801928/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Ndugu JOYCE NASON MWAMPONDELE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari kama ifuatavyo :
Aina ya gari : **FUSO**
Namba ya gari : **T 973 CEN**
Kwa yeyote atakayeiona anambwa kuripoti kituo vchochote cha polisi kilicho karibu. POLICE LOSS REPORT NAMBA :
**MBE/MBE/RB/801138/2020**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA**
**TAXATION CAUSE NO. 23/2019**
**(Arising from land case 19/2016)**

**KAGERA SUGAR LTD ..........................................DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**1. MARWA WANDWI ..................................JUDGEMENT DEBTOR**
**2. LINUS KAKIZA.........................................JUDGEMENT DEBTOR**
**3. MWANA GOZBERT KIBANTE .....................JUDGEMENT DEBTOR**
**4. ALFRED KAKWAYA ..................................JUDGEMENT DEBTOR**
**5. RUGEMALILA THABITI ............................JUDGEMENT DEBTOR**
**6. GERMANUS VYABUSA ............................JUDGEMENT DEBTOR**

**TO ALFRED KAKWAYA**

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Decree holder lodged Application against you and registered as **Taxation cause no 23/2019.**
Take Notice that the above said application has been fixed for mention on **3rd December 2020** at 8:30 Am before **Hon. J.M. MINDE DR** you are ordered to appear in person or through your Advocates.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of this Court this 16th **day of November, 2020.**

J.M. Minde
DEPUTY REGISTRAR
BUKOBA

116006302

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



1116006202

**SYLVIA TIMOTHY WILLIAM** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S 0233/0711** iliyotolewa na shule ya secondary ST MARY MAZINDE JUU mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/809083/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



116007302

**GIDEON MBETA RWEGERERA** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Master of Business Administration chenye namba **E0020513** kilichotolewa na Open University of Tanzania mwaka 2019. Transcript of Examination Result yenye namba **PG201610619** iliyotolewa na Open University of Tanzania mwaka 2019. Certificate of advanced Diploma in Information Technology kilichotolewa na Institute of Accountancy Arusha mwaka 2009. Academic Transcript for IAA Advance Diploma in Information Technology chenye namba **ADIT/00348/T.2005** iliyotolewa na Institute of Accountancy Arusha mwaka 2009. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi: Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/739843/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



116006402

**HASHIM WAKONGO KALALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4090/0293** kilichotolewa na NGARENARO SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/BUG/RB/809293/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ID'ECOR GLAZING LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA DYNA** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 759 DEQ.** Chassis namba **YY2110002099.** Engine namba **3YEAA2099.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/PHQ/RB/809480/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ID'ECOR GLAZING LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA DYNA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 369 DEP.** Chassis namba **YY2110007898.** Engine namba **3YEAA7898.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/PHQ/RB/809480/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



116006002

**ELIZABETH MAKEJA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0195-0004** kilichotolewa na shule ya secondary **ST. CAROLI** mwaka 2007, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa MW/RB/6966/2016**

## KUPOTEA KWA VYETI



116007302

**GIDEON MBETA RWEGERERA** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Postgraduate Diploma in Financial Management kilichotolewa na Institute of Accountancy Arusha mwaka 2011. Cheti cha Initial Teacher Education for Licenced Teachers chenye namba **0515** kilichotolewa na Ministry of Education and Culture mwaka 2004. Cheti cha kuzaliwa chenye namba **C No. 1000112125.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi: Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/739807/2020.**

## TAARIFA YA KUFUNGA BEFAO & CO (BFC) LTD

Tunapenda kuutarifu Umma kuwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika tarehe 15/04/2020 kiliazimia kufunga Kampuni ya **Befao & Co (BFC) Ltd** yenye Usajili. No. 135061 kuanzia tarehe **20/04/ 2020.** Kwa maelezo/madai wasiliana na Tel.
**0715-388297/0754-388297**
**au befao2017@gmail.com**

*Uza,*
*Chenye Thamani*
*Kubwa Kwa Kutangaza*
*Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Saba wafa wakidai aachiliwe Bobi Wine

**KAMPALA, Uganda**

IDADI ya waandamanaji waliofariki dunia wakati wa maandamano ya Jumatano ya kupinga kukamatwa kwa Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, imeongezeka na kufikia saba, polisi imesema.

Msemaji amezungumza na BBC jana na kusema kuwa zaidi ya waandamanaji 40 walijeruhiwa katika makabiliano na polisi.

Shirika la Msalaba Mwekundu Uganda, linasema kuwa wafanyakazi wake waliwasaidia watu 11 waliokuwa na majeraha ya kupigwa risasi.

Wakati huohuo, upinzani umesitisha kampeni zake kushinikiza kuachiliwa huru kwa Bobi Wine.

Waliokuwa majenerali wa jeshi, Mugisha Muntu na Henry Tumukunde pia wametaka polisi kusitisha unyanyasaji dhidi ya wagombea urais wa upinzani na raia.

Polisi imesitisha matukio kadhaa ya kampeni ya wagombea wa upinzani.

Bobi Wine alikamatwa katika mkutano wake wa kampeni mashariki mwa Uganda.

Polisi walimbeba Bobi Wine na kumweka kwenye gari lao wakidai kuwa amevutia umati mkubwa wa watu zaidi ya 200, kuliko idadi iliyopendekezwa na Tume ya Uchaguzi kama njia moja ya kukabiliana na virusi vya corona.

Mawakili wa Bobi Wine wanasema bado mteja wao hajafikishwa mahakamani.

*BBC*




Ghasia zikionekana katika baadhi ya mitaa nchini Uganda, huku ikidaiwa watu saba wamefariki dunia. Maandamano yalifanyika juzi, kupinga kukamatwa kwa mgombea wa urais, Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine. **PICHA/BBC**

# Rwanda kuwapima wanafunzi wote corona

**KIGALI, Rwanda**

SERIKALI ya Rwanda imeanza mkakati wa kupima kwa wingi virusi vya corona, katika shule mbalimbali nchini humo.

Wizara za Elimu na Afya ndizo zilizopewa jukumu la kusimamia zoezi hilo ambalo litatoa picha halisi ya maradhi hayo.

Taarifa zilizotolewa na wizara hizo zimeeleza kuwa zoezi hilo litafanyika kwa awamu na litazihusisha shule zote za msingi, sekondari na vyuo vikuu hasa kwenye maeneo ya nchi ambayo tayari yanaonekana kuwa na kiasi kikubwa cha maambukizi.

Ilieleza kuwa awamu ya kwanza itahusu kuchukua sampuli za wanafunzi elfu 2,500 wa shule za msingi mjini Kigali, sampuli za wanafunzi 2,000 wa shule za sekondari mjini na sampuli 500 za wanafunzi wa vyuo vikuu, kadhalika mjini Kigali na baadaye litaendelea nchi nzima.

Ni zoezi ambalo limeanza wiki mbili baada ya awamu ya kwanza ya shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu hasa wale waliokuwa wanakaribia kufanya mitihani yao ya mwisho wakati ulipozuka ugonjwa wa corona.

Waziri wa Elimu, Dk. Uwamaliya Valentine, alisema kwamba zoezi hili halitaathiri mchakato mzima wa masomo kwa sababu linafanyika kwa tahadhari kubwa.

"Kinachotarajiwa siyo kufunga shule zote nchini, isipokuwa tutajikita pale tutakapokuta kuna tatizo ndipo tutakapotilia mkazo na ndiyo maana kwa kila shule tumeandaa chumba cha dharura," alisema waziri wa elimu.

Kwa shule ambazo tayari zimeshafunguliwa wanafunzi na walimu wao walisema tahadhari inaendelea kwa kiwango cha juu.

Wizara ya afya inashikilia kwamba zoezi hili pia linalenga kufanya utafiti wa picha ya jinsi ugonjwa huo ulivyo shuleni.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Tiba nchini Rwanda, Dk. Sabin Nsanzimana, alisema: "Kwa siku hizi tunaona idadi ya maambukizi ikishuka, lakini kushuka kwa maambukizi hakuna maana kwamba virusi vimeisha, hapana isipokuwa tunaendelea kufanya utafiti ili kujua hata kule ambako vitakuwa vimejificha bila sisi kujua na ukipata maeneo walipo watu wengi lakini uchukue nafasi hiyo kujua hali ikoje".

Hadi kufikia juzi, watu 45 wameshafariki nchini Rwanda kutokana na ugonjwa wa Corona, huku maambukizi yakifikia watu 5,491 na waliopona wakiwa ni watu 5,004 huku wengine 442 wakiendelea kuuguzwa hospitalini.

*DW*

# Mchungaji atuhumiwa utakatishaji fedha

**LILONGWE, Malawi**

MCHUNGAJI aliyejitangaza kuwa nabii na kiongozi wa kanisa, Shepherd Bushiri, amejisalimisha kwa polisi nchini Malawi alikokuwa amekimbilia.

Bushiri anatafutwa kwa tuhuma za wizi na biashara haramu ya mzunguko wa fedha nchini Afrika Kusini.

Bushiri na mkewe Mary, walitoroka Afrika Kusini kwenda Malawi wiki iliyopita, wakikiuka masharti ya dhamana ambayo yalikuwa yamewekwa baada ya kukamatwa kwa kuhusika na kesi ya utakatishaji wa mamilioni ya fedha.

Bushiri alijisalimisha polisi Jumatano mjini Lilongwe. Msemaji wa Jeshi la Polisi, James Kadadzera, alisema kukamatwa kwake ni kwa kuitikia wito wa hati ya kukamatwa iliyotolewa na Shirika la Polisi la Kimataifa la Interpol.

"Na kwa kweli ilielezwa kwamba wawili hao wanashtakiwa nchini Afrika Kusini na wanaaminika kukiukia masharti ya dhamana yao, kwa hivyo, tulianzisha msako jana, na tuna hakika kwamba wenza hao walipata habari kwamba polisi wanawatafuta na sasa tunao chini ya ulinzi." Alisema Kadadzera.

Kadadzera alisema polisi walikuwa wakichukua taarifa kutoka kwao, lakini hawakujua ni lini watafikishwa mahakamani.

Bushiri ni nabii aliyejitangaza mwenyewe na kiongozi wa Kanisa lake la Enlightened Christian Gathering, ambalo linadai kuwa na matawi zaidi ya 70 ulimwenguni.

Nchini Afrika Kusini yeye, mkewe na wengine wawili wanatuhumiwa kuiba dola milioni 6.6 kupitia biashara haramu ya mzunguko wa fedha, na wizi.

Msemaji wa Bushiri, Ephraim Nyondo, alielezea sababu ya Bushiri kukimbilia Malawi.

"Kile nabii anachotaka ni hukumu ya haki nchini Afrika Kusini. Kumekuwa hakuna dalili ya yeye kuwa na kesi ya haki nchini humo," alisema Nyondo.

Kutoroka kwa Bushiri kuliambatana na ziara rasmi ya Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, nchini Afrika Kusini wiki iliyopita, ambayo ilichochea tuhuma kwamba rais huyo alikuwa sehemu ya mpango wa kuondoka kwa Bushiri.

Hii ilisababisha mzozo wa kidiplomasia wakati ndege ya Chakwera ilipozuiliwa katika Kituo cha Jeshi la Anga cha Waterkloof Ijumaa, siku hiyo hiyo ambayo Bushiri na mkewe walishindwa kuripoti kituo cha Polisi kwa dhamana.

Sheriff Kaisi ni mhadhiri wa sayansi ya siasa katika Chuo Kikuu cha Blantyre.

Aliiambia VOA kwamba kukamatwa kwa Bushiri kunapasa kumaliza mzozo wa kidiplomasia.

**VOA**



# JOVIC

## ANA MABAO MENGI SERBIA KULIKO MADRID

**MADRID, Hispania**

LUKA Jovic amekuwa na wakati mgumu tangu alipojiunga na Real Madrid mwaka jana, lakini nyota huyo wa Serbia anapokuwa na timu ya taifa mambo yanakuwa tofauti kabisa.

Jovic alisajiliwa kutoka kwa miamba wa Bundesliga, Eintracht Frankfurt kwenda Madrid kwa euro milioni 60 mwaka 2019, hata hivyo amefunga mabao mawili tu katika mechi 32 kwa mabingwa hao wa LaLiga.

Pamoja na kuwa na wakati mgumu kwa timu hiyo ya mji mkuu wa Hispania, Jovic alionyesha kiwango cha juu wakati aliporudi kuichezea Serbia kwenye mapumziko ya mechi za kimataifa.

Baada ya kuifungia Serbia kwenye mashindano ya kombe la kufuzu Euro 2020 (sasa zitacheza 2021), wiki iliyopita dhidi ya Scotland, Jovic alifunga mara mbili wakati wakiifumua Urusi 5-0 kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa, Jumatano.

Kwa kupachika mabao matatu kwa kikosi cha Serbia, inamaana, Jovic ana mabao mengi zaidi kwenye timu ya taifa kuliko kwa kipindi chote alichowachezea Los Blancos.


Jovic hajaifungia Madrid tangu wakati wa ushindi wa mabao 4-1 kwenye LaLiga wakati wakiifumua Osasuna Februari, mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ameanza mara mbili katika mechi nne za Ligi Kuu Hispania kwa Madrid kwa msimu huu 2020-21, huku akipiga shuti moja tu lililolenga goli.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jovic amecheza mechi moja na kama ilivyo kwenye LaLiga, amepiga shuti moja tu lililolenga goli kwa kikosi hicho cha Zinedine Zidane.

## GREALISH AKUBALI KUFANANISHWA NA GAZZA

**LONDON, England**



KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, Jack Grealish amekubali kulinganishwa na Paul Gascoigne 'Gazza' baada ya kuendelea kuwa na kiwango cha kuvutia dhidi ya Iceland.

Grealish aliisaidia England kumaliza michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa ngazi ya makundi wakati ikiibuka na ushindi wa 4-0 pale kwenye dimba la Wembley, Jumatano.

Nyota huyo wa Aston Villa alipiga pasi tatu muhimu na alifanyiwa faulo mara sita nyingi zaidi kuliko mchezaji yoyote wakati Phil Foden akifunga mara mbili baada ya mabao kutoka kwa Declan Rice na Mason Mount.

Huku akiwa analinganishwa na nyota wa zamani wa England, Gazza, Grealish alikubali ulinganisho huo, lakini alisema bado ana kazi kubwa ya kufanya.

"Naukaribisha mlinganisho huo. Nampenda Gazza. Niliangalia makala yake kwenye televisheni zaidi ya mara milioni," alisema.

"Napenda staili yake, ndani ya uwanja na nje ya uwanja. Napenda namna alivyokuwa akicheza soka, soka la kuvutia na kufurahisha.

"Unajua nimesikia mengi kuhusu yeye yakisemwa na ilikuwa furaha kwangu kumtazama."

## FABREGAS: SIZUNGUMZI NA GUARDIOLA

**MONACO, Ufaransa**

CESC Fabregas bado anamchukulia kocha wa zamani wa Chelsea, Jose Mourinho "ni rafiki" lakini amebainisha hazungumzi na Pep Guardiola licha ya kumchukulia kama mtu aliyemvutia zaidi wakati anakua kisoka.

Fabregas kwa sasa na umri wa miaka 33 na anacheza Monaco, amekuwa mmoja wa viungo wanaotambulika zaidi duniani baada ya kujitambulisha yeye mwenyewe katika kikosi cha kwanza cha Arsenal akiwa na umri wa miaka 16, mwaka 2003.

Tangu hapo amekuwa na kiwango cha kuvutia kabla ya kurudi tena Barcelona - ambako ndiko alikolelewa na kukulia chini ya Guardiola, akishinda mataji sita kwa misimu mitatu.

"Mourinho alikuwa mmoja wa watu walionivutia sana mimi, na nikaondoka Barca," alisema Fabregas akiiambia Tot Costa.

"Aliniambia kwamba alikuwa ananifuatilia sana wakati akiwa Chelsea na mimi nikiwa Arsenal, na baadaye tukawa tunafanya wote mazoezi pale Real Madrid wakati nikiwa Barcelona."

Lakini Fabregas amesema licha ya Guardiola kuwa ndiye mtu aliyemvutia zaidi yeye, walipofanya kazi pamoja hawakuwa na mahusiano mazuri.

"Sijazungumza na Guardiola muda mrefu sana," amesema.

"Kuna vitu vilitokea kati yangu mimi na yeye na siwezi kuviweka wazi kwa sasa.

"Yeye ndiye mtu aliyenivutia zaidi wakati nikiwa mdogo na nilijifunza mengi kutoka kwake kama mchezaji, lakini sio rafiki tangu."





# MANCINI

## KUPANGA KIKOSI CHA ITALIA NI KAZI

**ROME, Italia**

ROBERTO Mancini alisifia vipaji vya wachezaji wachanga kwa kikosi cha Italia na anatambua "tatizo kubwa" linalowakabili kwenye michuano ya Euro 2020 inayokuja.

Michuano ya Euro 2020 itachezwa Juni mwakani, baada ya mlipuko wa virusi vya corona kuvuruga ratiba.

Kocha huyo kuu wa Italia, Mancini alikosa mechi zote tatu mwezi huu, baada ya kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona na hivyo kutakiwa kujitenga.

Kocha Msaidizi, Alberigo Evani ameiongoza Azzurri katika ushindi wa mechi tatu bila kuruhusu bao, huku Jumatano wakiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Bosnia-Herzegovina na kushuhudia kikosi chake kikitinga fainali ya timu nne ya Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Kikosi hicho cha Mancini kitakuwa kwenye mashindano ya Euro 2020 yanayofanyika Juni mwakani.

Italia ilishuhudia wachezaji wengi wakiondolewa kwenye kikosi hicho mwezi huu kutokana na matatizo mbalimbali, wakiwamo Leonardo Bonucci, Giorgio Chiellini na Marco Verratti, lakini Mancini hana shaka na kiwango cha timu hiyo.

"Kuchagua wachezaji 23 kwa ajili ya Euro 2020 litakuwa tatizo kubwa," amesema Mancini akiambia Rai Sport.

"Tayari limekuwa jambo gumu kwa sababu wachezaji wengi wameonyesha kiwango cha kuvutia, hivyo nitakuwa kwenye wakati mgumu sana kuchagua wachezaji 23 wa mwisho."

# DE BRUYNE ATAKA KIWANGO UBELGIJI

**LEUVEN, Ubelgiji**



KEVIN De Bruyne amesema Ubelgiji inahitaji kuwa na kiwango cha mwendelezo baada ya ushindi wa 4-2 kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Denmark.

Kikosi hicho cha Roberto Martinez, kilipata pointi zote tatu mjini Leuven na hivyo kufuzu kwenye fainali ya timu nne mwakani.

Youri Tielemans aliiweka Ubelgiji mbele, lakini Jonas Wind akasawazisha na Martin Braithwaite angeweza kufunga jingine katika kipindi cha kwanza wakati Denmark walipotawala mchezo.

Baadaye Ubelgiji wakatawala mchezo na Romelu Lukaku akafunga mara mbili na De Bruyne akaongeza moja dakika za majeruhi baada ya golikipa Thibaut Courtois kufanya makosa ya kushindwa kuokoa pasi ya Nacer Chadli na ikajaa wavuni mwake.

Ubelgiji hawakuwa na kiwango cha kuvutia wakitengeneza nafasi chache kipindi cha kwanza, lakini walionekana kuamka kipindi cha pili, huku Denmark wakitawala kipindi cha kwanza.

Na De Bruyne sasa anataka Ubelgiji kuendelea kuwa na kiwango kile kile, ili kupata matokeo mazuri zaidi uwanjani.

"Tunatakiwa kuwa na kiwango kile kile," alisema nyota huyo wa zamani wa Manchester City, akinukuliwa na Het Nieuwsblad.

"Denmark walicheza vizuri zaidi kipindi cha kwanza. Sisi hatukucheza vizuri kabla ya kubadilika kipindi cha pili.

"Tunatakiwa kuendelea kuwa kwenye kiwango hiki hiki, maana kiwango cha timu ndio jambo la muhimu zaidi kwa sasa."



# WIJNALDUM: UHOLANZI INATAKIWA KUJIIMARISHA

**CHORZOW, Poland**

GEORGINIO Wijnaldum anatambua kuna wakati Uholanzi haikuwa kwenye kiwango cha kuvutia wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Poland.

Uholanzi ilitoka nyuma na kupata ushindi wa 2-1 mjini Chorzow, lakini haikuwasaidia kufuzu kwenye fainali ya ya mwisho ya mashindano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA, baada ya Italia kupata ushindi wa 2-0 dhidi ya Bosnia-Herzegovina na kuwahakikishia kumaliza nafasi ya kwanza katika Kundi A1.

Kamil Jozwiak aliiwezesha Poland mbele katika dakika ya tano kwa bao la kuvutia, lakini Wijnaldum alishinda penalti ambayo ilifungwa na Memphis Depay dakika ya 77 na baadaye akafunga bao la pili kwa kichwa na kumpa kocha Ronald de Boer ushindi wa pili tangu achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo.

Poland walikuwa na nafasi kubwa ya kushinda mchezo huo, amebainisha Wijnaldum na kutaka Uholanzi kujiimarisha zaidi kuelekea michuano ya Euro 2020.

"Nafikiri hii ilikuwa moja ya mechi bora zaidi. Mwanzoni hatukuwa wakali na walikuwa na uwezo wa kufunga mapema, lakini mchezo ulikuwa mzuri," amesema Wijnaldum akiiambia NOS.

"Tunatakiwa kufanya vizuri zaidi, maana kwa upande mwingine ni kama tulizidiwa kiwango na sasa tunatakiwa kujipanga.

"Kuna wakati tulionekana kama tumerudi kwenye ubora, lakini mambo haraka yalibadilika na hivyo lazima tubadilike."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI: NIMECHOKA KUBEBESHWA LAWAMA

## Nahodha huyo akerwa kuonekana yeye ndiyo chanzo cha kila tatizo linalotokea Barca...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amemjibu mwakilishi wa zamani wa Antoine Griezmann, baada ya kudai nahodha huyo wa Barcelona ndio sababu kubwa kwa nyota huyo wa Ufaransa kuwa na wakati mgumu pale Camp Nou.

Mshauri wa zamani wa Griezmann, Eric Olhats alinukuliwa na gazeti la France Football wiki iliyopita akisema kwamba, Messi ambaye alidai "ana nguvu ya kila kitu" pale Barca - hakutaka Griezmann asajiliwe na "kumfanya ajihisi kutokaribishwa vizuri ".

Messi alirudi Barcelona Jumatano baada ya kuiwakilisha Argentina kwenye mechi za kufuzu Kombe la Dunia na aliulizwa kuhusu kauli hiyo wakati akiondoka uwanja wa ndege wa El Prat.

Alisema: "Nimechoka mara zote mimi kuambiwa ndio chanzo cha matatizo yote klabuni."

Barca ilimsajili Griezmann kutoka Atletico Madrid kwa euro milioni 120 Julai, 2019, lakini ameshindwa kufikia matarajio ya wengi.

Amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 42 za LaLiga kwa Blaugrana hao, akiwa na wastani wa bao moja kila baada ya dakika 273.

Kwa misimu mitano kule Atletico, Griezmann alifunga bao kila baada ya dakika 152.

Tangu Griezmann ajiunge na Barca, Messi amefunga mabao 28 na kutoa pasi za mwisho 21 kwenye LaLiga.

Nyota huyo wa Argentina amekuwa kwenye sintofahamu baada ya kushindwa kulazimisha kuondoka msimu uliopita pale Barca, ambako mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Katika mahojiano hayo, Olhats aliongeza: "(Messi) ni kama mfalme hakuutaka usajili wa Antoine.

"Mtazamo wake ulikuwa wazi kabisa, hakutaka kusikia usajili wake, mara zote nachukizwa na kauli yake akisema kwamba hana tatizo lolote na Griezmann.

"Msimu uliopita, wakati Griezmann alipowasili, Messi hakuzungumza naye na hakuwa anampasia mpira.

## KWA UFUPI

**LIVERPOOL, UNITED VITANI**

LIVERPOOL na Manchester United zinawania kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22, ambaye anawindwa na Bayern Munich 22. ***(Bild, via Mirror)***

**VARANE ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United wana fursa ya kumsajili kiungo wa kati, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 27 na raia wa Ufaransa kutoka Real Madrid. ***(Manchester Evening News)***

**WIJNALDUM AGOMBEWA**

REAL Madrid wanakabiliana na ushindani kutoka kwa Barcelona katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya kiungo wa kati wa Liverpool, Mholanzi, Georginio Wijnaldum ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Corriere Dello Sport via Sport)***

**MESSI NJIA MOJA CITY**

LIONEL Messi amewawashia taa ya kijani Manchester City kwenye mbio za kuwania kumsajili, baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 33, kusema kuwa "amechoka yeye kila siku kuonekana tatizo" katika klabu ya Barcelona. ***(Express)***

**ALABA KUMRITHI RAMOS**

MLINZI wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28 ndiye mchezaji anayelengwa zaidi na Real Madrid kama Sergio Ramos ataondoka katika klabu hiyo msimu huu. ***(AS)***

**ANDERSON KUREJEA WEST**

WINGA wa West Ham, Felipe Anderson (27), anaweza kurejea mapema kutoka Porto kama timu hiyo ya Ligi Kuu Ureno itaweza kumsajili tena mshambuliaji Mbrazil, Hulk mwenye miaka 34, kutoka timu ya Shanghai SIPG Januari. ***(Record - in Portuguese)***

**BARCA YAMPOTEZEA GRACIA**

KLABU ya Barcelona inaonekana haipo tayari kumsajili mlinzi wa pembeni, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, huku Manchester City anakocheza sasa wakiwa tayari kutokubali thamani anayopewa mchezaji huyo ya euro milioni 20. ***(Marca)***

**REKIK KUTUA ARSENAL**

ARSENAL wamekubali kumpa mkataba Mtunisia anayechea timu ya vijana ya umri chini ya miaka 21, Omar Rekik (18), kutoka Hertha Berlin ifikapo Januari mwakani na kumtoa kwa mkopo kwa timu hiyo ya Ujerumani. ***(Football London)***

**CORK AGEUKA LULU**

KLABU za Sevilla na Hertha Berlin zipo kwenye mbio moja za kuwania kumsajili mlinzi wa Paris St-Germain na Sheffield United, Jack Cork mwenye umri wa miaka 31 anayecheza kule Bunrley. ***(Mirror)***

**KLOPP AWABEBA VIJANA**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amewapa fursa wachezaji wanane kutoka chuo cha mafunzo ya soka wakati wa mazoezi wiki hii, huku timu hiyo ikikabiliwa na changamoto cha wachezaji wanaoendelea kuuguza majeraha. ***(Mirror)***

**XAVI ATABIRIWA MAKUBWA**

NYOTA wa zamani wa Barcelona, Xavi anaweza kuwa 'Sir Alex Ferguson' wa klabu hiyo kama atarejea kama kocha, anasema mgombea wa kiti cha urais wa timu hiyo, Victor Font. ***(Reuters)***

HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION YAIWAHI MAPEMA SIMBA ARUSHA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumaliza majukumu ya kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amekiongeza kikosi chake kutua Arusha tayari kuwasubiri Simba kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili, Mgunda ambaye ni Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, alisema kuwa tayari anaendelea na maandalizi ya mchezo huo ambao anaamini utakuwa mgumu kwa pande zote mbili.

Mgunda alisema timu yake imejipanga kufanya vyema katika mechi hiyo ya raundi ya 11 na kuendelea kujiweka kwenye nafasi nzuri.

"Vijana nimewakuta wapo vizuri na tunakwenda kupambana kwenye mechi ngumu. Tutacheza na timu ngumu, yenye wachezaji wazuri na natarajia mchezo pia utakuwa mzuri," alisema Mgunda, straika wa zamani wa Coastal Union.

Kocha huyo alikuwa jijini Dar es Salaam na kikosi cha Stars ambacho kilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Tunisia katika mechi ya Kundi J ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022), zitakazofanyika nchini Cameroon.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Coastal Union inashika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 12 baada ya kushinda mechi tatu, sare tatu na kupoteza michezo minne.

Kikosi cha mabingwa watetezi, Simba kilichoko chini ya Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck na Suleiman Matola kinatarajia kutua Arusha leo.

Baada ya mchezo huo, Simba iliyoko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 20, itaendelea na maandalizi ya mechi yake ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau FC ya Nigeria.



Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuf Singo (kushoto), akimkabidhi seti ya jezi pamoja na mpira, Mwalimu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Malya kilichoko jijini Mwanza, Consolatha Luhende (kulia), kwenye hafla ya uzinduzi wa Programu ya Mpira Fursa iliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Karibu Tanzania Organization (KTO). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mpira Fursa kuwabeba wanawake

**Na Jumanne Juma**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Karibu Tanzania Organization (KTO), linalofanya shughuli zake kama mwamvuli wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), limezindua rasmi programu ya mafunzo ya maendeleo ya soka kwa wanawake vijana ijulikanayo kama "Mpira Fursa".

Mkurugenzi wa KTO, Maggid Mjengwa, alisema jana jijini Dar es Salaam nia ya kufanya mafunzo hayo ya siku nne ni kuwajengea uwezo washiriki ili kwenda kufundisha michezo kwa wanafunzi wa kike wa shule za msingi.

Mjengwa alisema Mpira Fursa ni programu iliyoanzishwa na inayoendeshwa na KTO kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), pamoja na vyuo 43 vya maendeleo ya wananchi vikiwamo 41 vinavyotekeleza programu ya maarifa kwa wanawake vijana waliokatishwa masomo kutokana na sababu mbalimbali.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuf Singo, ameishukuru KTO na kutoa hamasa kwa walimu wa michezo waliopata mafunzo na kuwakumbusha kwenda kuyafanyia kazi kwa walengwa.

Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Dk. Noel Mbonde, alisema Mpira Fursa ni programu nzuri ambayo imewaendelea wanawake ambao walikatishwa ndoto zao.

Mbonde alisema kwa kutumia mpira wa miguu, taasisi hiyo imewashirikisha wanawake na kuwasaidia kujikomboa kupitia mchezo huo.

Pia mkuu wa programu hiyo, Mia Mjengwa alisema programu hiyo imelenga kusapoti jitihada za serikali katika kumwinua mwanamke katika kupata fursa kwa sababu mpira ni ajira na humpa nguvu ya kutambua haki zake.

## Sureboy, Masai kuikosa KMC FC

**Na Saada Akida**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC itawakosa nyota wake wawili, Salum Aboubakar 'Sure Boy' na beki Oscar Masai katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wachezaji hao ni majeruhi na wameondolewa kwenye mipango ya mechi hiyo.

Vivier alisema Sure Boy alipata maumivu ya kidole cha mguu akiwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) na kutakiwa kukaa nje kwa muda wa siku 10 wakati Masai aliyeumia enka tayari ameanza mazoezi mepesi.

Kocha huyo alisema wachezaji wengine wako fiti na wanatumia siku mbili (jana na leo), kuweka mambo sawa ili kuwa tayari kupambana kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Walikuwa katika majukumu ya timu zao za Taifa, wamerejea kambini isipokuwa nyota wawili, Prince Dube aliyetarajiwa kutua nchini usiku wa leo (jana) na beki wao Mganda Nicholas Wadada anayetarajiwa kuingia kesho (leo), mchana," Vivier alisema.

Aliongeza wanatarajia kukutana na ushindani katika mchezo huo kutokana na rekodi nzuri ya KMC inapokuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani.

"Ila Dube atatua nchini wakati wowote kuanzia jioni ya leo (jana), tutakuwa naye kwenye mchezo huo muhimu, tunahitaji kuendelea kupata ushindi na kujiimarisha kileleni," aliongeza kocha huyo.

Azam FC wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 25 wakati wenyeji wao KMC, wenyewe wana pointi 15 na wako katika nafasi ya sita.

## Dodoma Jiji FC yarejea nyumbani

**Na Adam Fungamwango**


TIMU ya Dodoma Jiji FC inarejea rasmi kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Jamhuri Dodoma wakati itakapowakaribisha Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Johnson Fortunatus, alisema jana wanafurahi kurejea kwenye uwanja wa nyumbani ambao wameuzoea na wanatarajia kufanya vyema katika mechi hiyo.

"Kwanza tunashukuru Mungu kupewa taarifa na Bodi ya Ligi ya kuutumia tena Uwanja wa Jamhuri Dodoma. Hapa ndipo nyumbani kwetu. Iringa ni Iringa na Dodoma ni Dodoma. Sisi hatukuwa na mapumziko kipindi chote hiki. Tuliwaambia benchi la ufundi hakutakuwa na mapumziko, badala yake mazoezi yaendelee, waangalie mapungufu yaliyojitokeza na kuyarekebisha," alisema Fortunatus.

Kiongozi huyo alieleza hawakufurahishwa na matokeo ya mechi tatu zilizopita, na sasa wamerudi nyumbani kurekebisha pale walipoharibu. "Kuna mechi kama tatu hivi hatukufanya vizuri, tumeona tulipokosea, tumeyafanyia kazi makosa yetu, tunatarajia kushinda mechi hii," aliongeza katibu huyo. Uwanja wa Jamhuri ulisitishwa kuchezewa ligi kupisha shughuli za kitaifa na mechi zake kuhamishiwa kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Michezo
Ijumaa Novemba 20, 2020
Nipashe



MESSI: NIMECHOKA KUBEBESHWA LAWAMA HABARI UK 22



Straika wa Timu ya Taifa ya England, Jack Grealish (kulia), akijaribu kumtoka beki wa Ice Land, Victor Palsson, katika mechi ya Kundi la Pili ya Ligi ya Mataifa Ulaya iliyochezwa kwenye Uwanja wa Wembley, jijini London juzi usiku. England ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# KAZE ATANGAZA DK. 180 HATARI

## Ni katika mpango maalum wa kugawa 'dozi' dhidi ya Namungo, Azam FC...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kalenda ya kimataifa kumalizika, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema analiandalia programu maalumu tatizo la ushambuliaji kuelekea mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata za timu hiyo.

Yanga inatarajia kuwakaribisha Namungo FC keshokutwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na Novemba 25, mwaka huu itakutana na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaze alisema baada ya kucheza mechi mbalimbali za kirafiki, amebaini washambuliaji wake wanakosa nguvu zaidi za kupambana lakini pia wakipokonywa kirahisi mipira na mabeki wa timu pinzani.

Kaze alisema amegundua tatizo hilo na tayari ameshaanza kulifanyia kazi na anaamini mabadiliko ya washambuliaji wake yataonekana kwenye mechi zao mbili zinazofuata hivi karibuni. "Hizi mechi za kirafiki zimenisaidia kufanyia kazi upungufu wa kikosi, awali ilikuwa kuna tatizo la viungo kufikisha kwa usahihi mipira kwa washambuliaji, ila sasa limebaki suala na wafungaji kutowapa purukushani mabeki wa timu pinzani.

Nimefanyia kazi hilo kwa kuwapa majukumu washambuliaji katika maandalizi ya mechi yetu dhidi ya Namungo, tuhakikishe wanajitahidi kutumia vizuri nafasi wanazopata na huku wakipeleka presha kwa mabeki wa wapinzani wetu," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema pia kikosi chake kinaendelea vizuri na tayari baadhi ya nyota wake waliokuwa majeruhi wako vyema na wanatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi kitakachopambana na wawakilishi hao wa Bara kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Aliwataja nyota hao waliorejea kikosini ni pamoja na beki wa kati tegemeo, Lamine Moro na Carlos Carlinhos.

"Carlinhos yupo fiti baada ya kumpa nafasi katika mechi ya kirafiki dhidi ya African Lyon, ni miongoni mwa nyota ambao watakuwa katika mipango yangu ya mechi ijayo dhidi ya Namungo," alisema kocha huyo.

Aliongeza bado wana kazi kubwa ya kufanya vizuri kwenye ligi hiyo na ana imani wataendelea kupata matokeo mazuri ndani ya uwanja nyumbani kwa sababu wachezaji wote wapo tayari kwa mapambano.

Kikosi cha Yanga kimeweka kambi Kigamboni jijini na kinaendelea na mazoezi yake kuelekea michezo hiyo ya ligi inayowakabili kuanzia keshokutwa.

# `MO DEWJI AMTAJA 'MCHAWI' WA SOKA

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Mohammed Dewji 'Mo', amesema endapo rushwa michezoni 'itafumbiwa macho', soka la Tanzania halitaendelea.

Mo alisema hayo katika hafla ya chakula cha usiku iliyoandaliwa na wanachama wa Simba wa Tawi la Bunge 'Simba Mjengoni', yenye lengo la kukutana na viongozi mbalimbali wa timu hiyo.

"Tabia ya rushwa michezoni, kununua waamuzi na hujuma haviwezi kuendeleza soka letu, mageuzi katika mifumo wa uendelezaji wa vilabu vyetu ndio jawabu, maana klabu zetu lazima zizaliwe upya kama inavyofanya Simba ili soka letu liende mbele na la Tanzania pia," alisema Mo.

Mwenyekiti huyo alisema klabu hiyo ina mpango wa kuwa na timu za vijana za umri chini ya miaka 18, 17, 16 na 15 na wanatarajia kuzunguka kila mkoa ili kusaka vipaji hivyo.

"Tunaenda mkoa kwa mkoa kusaka vipaji, tutawaleta na kuwasomesha na kutafuta familia ya kukaa nao ili kuwajenga kinidhamu, kidini," alisema mwekezaji huyo.

Aliwatoa hofu wanachama na mashabiki juu ya uwekezaji wake wa Sh. bilioni 20 na kueleza mambo yatakapokuwa sawa, watafikia tamati ya mjadala huo.

"Napenda kuwatoa hofu kuhusu Sh. bilioni 20, hakuna haja ya kuwa na hofu. Simba kwangu sio biashara bali ni familia kwanza. Mapenzi yangu kwa Simba hayapimiki kwa fedha. Matamanio yangu ni Simba kufanikiwa kimataifa,"aliongeza.

Alisema pia malengo ya Simba yamegawanyika katika hatua tatu, kwanza ikiwa ni mpango wa muda mfupi wa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Bara, pili kudhamiria kujenga klabu endelevu na malengo ya muda mrefu ni kushinda taji la ubingwa wa Afrika.

Naye, Mwenyekiti wa Tawi la Simba Mjengoni, Rashid Shangazi, alisema kuna tatizo la ukiritimba wa idara na taasisi za serikali, na baadhi ya viongozi wa serikali kutokuwa na mtizamo chanya kuhusu masuala ya uwekezaji katika soka.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002